**MALORI** 250 ya Tanzania yazuiwa DRC madai ya kodi



UKURASA 2

**WAZIRI** Mkuu anadi vivutio uwekezaji Italia



UKURASA 3

**ISRAEL** yabariki misaada Gaza kwa masharti

UKURASA 19



**NEYMAR NJE YA UWANJA MIEZI NANE**

UKURASA 21


# Nipashe

Ijumaa Oktoba 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581469

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## Kampuni kupunguza wafanyakazi 500 SGR

UKURASA 8

MAKALI YA PETROL

# Wenye magari wakimbilia gesi

UKURASA 2



## Papa ateua maaskofu Njombe, Bukoba

UKURASA 2



Papa Francisco



Askofu Eusebio Kyando



Askofu Jovitus Mwijage

UKURASA WA 24

## SIMBA YAPANIA KUIHESHIMISHA NCHI LEO

SIKU ambayo ilikuwa ikisubiriwa na wadau wengi wa soka Barani Afrika imefika ambapo leo wawakilishi wa Tanzania na Afrika Mashariki klabu ya Simba itaumana na wawakilishi wa Afrika Kaskazini na mabingwa wa Misri, Al Ahly kwenye mchezo wa ufunguzi wa michuano...



**MICHEZO** **GAMONDI, DABO WATAMBIANA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Malori Tanzania yazuiwa DRC madai ya kodi

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya malori ya mizigo 250 ya Tanzania yanashikiliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa madai kwamba kampuni za madini ambazo huchukua mzigo kwao yanadaiwa kodi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori wa Kati na Wadogo Tanzania (TAMSTOA), Chuki Shabani, alisema malori hayo yamezuiwa kwa zaidi ya siku tatu huku madereva wake wakiishi katika wakati mgumu na wao kuendelea kupata hasara.

"Huenda hata sasa idadi ya malori yanayozuiwa imeongezeka. Kwa leo (jana) siko ofisini lakini idadi hiyo niliyokutajia ni ya siku tatu zilizopita," alisema Shabani.

Alisema malori hayo yanazuiliwa kwenye eneo la mgodi linalojulikana kama Wiski Kasumbaresa lililoko kwenye mpaka wa kati ya Congo na Zambia.

"Migodi iko mingi ambako malori yetu huchukua madini na yalipoanza kuzuiwa ni huko Kasumbaresa lakini tunaambiwa kuna migodi mingine miwili nako yanazuiliwa na inadaiwa kwamba migodi hiyo inadaiwa kodi na serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

"Kinachotushangaza ni kwamba badala ya kushusha mizigo ambayo imepakia kwenye malori yetu na wakayaachia yaende, wao wanayashikilia. Hivi ninavyokwambia hali ni mbaya kwa madereva kwa sababu eneo hilo halina huduma za kijamii kwa hiyo wanaathirika sana," alisisiza.

Kiongozi huyo alisema kushikiliwa kwa malori hayo kunasababisha athari za kiuchumi kwa kuwa, madereva wanataka walipe stahiki zao.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Balozi wa Tanzania nchini Congo, Said Mshana, alisema wanaendelea kushughulikia tatizo hilo.

"Taarifa za kushikiliwa kwa malori hayo tunazo na si kutoka Tanzania pekee bali kuna hata ya Zambia na Zimbabwe, hivyo changamoto hiyo tunaifahamu na tunaifanyia kazi kwa kutumia njia za kidiplomasia.

"Muhimu hapa ni kampuni zinazodaiwa kodi na serikali ya Congo zimetakiwa kutokuendelea na shughuli zake hadi hapo watakapolipa kodi," alisema Balozi Mshana



Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle (kushoto) na Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji wakitia saini hati ya makubaliano ya majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), Leodegar Tenga (kulia), Ofisa Biashara Mwandamizi wa Ubalozi huo, Aliza Totayo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenye magari wakimbilia mfumo wa gesi

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema mwitikio wa watu kubadilisha magari yao kutoka matumizi ya petroli kwenda kwenye gesi umekuwa mkubwa na mpaka sasa magari yaliyobadilishwa mfumo yamefika 3,000.

Shirika hilo limesema magari ambayo yamewekwa mfumo wa matumizi ya gesi yatatakiwa kufanyiwa ukaguzi mara mbili kwa mwaka na maofisa wake vinginevyo hayataruhusiwa kujaza gesi kwenye kituo chochote nchini.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Viwango wa Shirika hilo, Anold Mato, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mchakato unaoendelea wa kubadilisha magari yanayotumia mafuta kwenda kwenye matumizi ya gesi.

Alisema ukaguzi huo utakuwa unafanywa na maofisa wa shirika hilo ambao wamepewa mafunzo maalum kuhusu ukaguzi wa mifumo hiyo ya gesi na kufaulu mitihani iliyoandaliwa na shirika hilo.

Alisema ukaguzi huo ni muhimu kwa kuwa mitungi inayowekwa gesi hiyo huwekwa mkandamizo mkubwa ili kumwezesha mtumiaji kwenda umbali mrefu kabla hajajaza tena.

Alisema ingawa mitungi hiyo hujazwa kwa mkandamizo mkubwa, lakini uwezekano wa kulipuka ni mdogo sana kulinganisha na gesi inayotumika majumbani.

Alisema vifaa vinavyotumika kubadilisha mfumo huo vimekaguliwa na TBS na kwamba ni salama kwasababu ndivyo vinavyotumika kwenye nchi ambazo zilishaanza kutumia gesi kwenye magari muda mrefu.

"Vifaa ambavyo vinaletwa kubadilisha mfumo wa magari yetu kwenda kwenye matumizi ya gesi ni salama kabisa kwasababu vinatoka kwa wenzetu ambao walishaanza kwa hiyo utamaduni wa kufanya ukaguzi mara mbili kwa mwaka ni wa kimataifa siyo wa hapa tu," alisema.

"Na lengo ni kujiridhisha kama mfumo uliowekwa bado uko madhubuti kwaajili ya matumizi yaliyolengwa na kama kuna tatizo lifanyiwe marekebisho mapema kwa hiyo ambaye hatalifanyia ukaguzi gari lake ajue hatajaziwa gesi kwa kuwa hilo ni muhimu kwa usalama wa gari," alisema.

Alisema, kwa kuwa matumizi ya mitungi hiyo ya gesi kwa hapa nchini ni suala jipya, TBS imekataza kuingizwa mitungi ambayo imeshatumika na badala yake wanaruhusu mitungi mipya kwa kuwa ni vigumu kutambua kwamba ile iliyokwishatumika ilitumika kwa muda gani.

"Mitungi hii ina ukomo wake wa matumizi tangu ilipotengenezwa kuna mingine ukomo wake ni miaka 20, mingine miaka 30 na mzalishaji wa hii mitungi lazima aandike imetengenezwa na nani, lini, kujaza presha kiwango gani na ukomo wake ni lini," alisema.

Yona Afrika ambaye ni Meneja wa Viwango wa (TBS), alisema utaratibu wa kubadili mifumo ya mafuta kwenda kwenye gesi ilianza tangu mwaka 2010 na wakati huo kampuni zilizokuwa zikifanyakazi hiyo zilikuwa mbili pekee, lakini sasa ziko tano Dar es Salaam.

Alisema gari lililobadilishwa kutoka kwenye matumizi ya mafuta kwenda kwenye gesi, mfumo wake wa mwanzo unabaki vile vile na gesi itakapoisha mwenye gari anaweza kurejea kwenye mfumo wake wa mafuta.

"Na kwa viwango ambavyo tumeviweka mpaka sasa hakuna athari yoyote kwa watu ambao magari yao yamebadilishwa kutoka kwenye mafuta kwenda kwenye matumizi ya gesi kwahiyo tuwaondoe wasiwasi wale wanaotaka kwenda kubadilisha mfumo," alisema.

Alisema kuna magari ambayo yametengezwa yakiwa maalum kwa kutumia gesi pekee wakati kuna yaliyotengenezwa yakiwa na mifumo yote miwili ya gesi na mafuta.

"Pia kuna magari yanayotumia gesi na umeme, kwahiyo ni hiyari mtumiaji atumie nishati gani, sasa kwenye kubadilisha magari kutumia gesi tunaangalia vifaa vinavyotumika na vingi vinatoka nje ya nchi na jukumu la kudhibiti hivyo vifaa ni letu TBS," alisema.

Kadhalika, TBS imekuwa ikisisitiza vifaa hivyo vikaguliwe nje ya nchi kwa kampuni ambazo zinafanyakazi na shirika hilo ili visichelewe kutoka bandarini kutokana na taratibu za ukaguzi.

"Lakini kama hujakagua huko nje tutakagua hapahapa nchini ila hatupendelei sana ukaguzi ufanyike hapa tunapenda ufanyike nje ya nchi ili kupunguza mlolongo wakati wa kuvitoa bandarini," alisema.

# Papa ateua maaskofu wapya Njombe, Bukoba

**Na Restuta James**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Baba Mtakatifu Fransisko, amewateua mapadre Eusebio Kyando na Jovitus Mwijage kuwa maaskofu wa majimbo ya Njombe na Bukoba.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Padre Charles Kitima, alisema uteuzi huo ulianza jana na kwamba watawekwa wakfu miezi miwili ijayo.

Alisema Askofu Mteule Kyando anachukua nafasi ya Askofu Alfred Maluma, aliyefariki dunia Aprili 6, mwaka juzi. Askofu Maluma aliteuliwa kuongoza jimbo la Njombe Juni 8, 2002 na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II.

Dk. Kitima alisema Askofu Mteule Mwijage anachukua nafasi ya Askofu Desiderius Rwoma ambaye amestaafu. Askofu Mstaafu Rwoma alishika kiti hicho kwa miaka 23 akianzia Jimbo la Singida na baadaye Bukoba, hadi alipoomba kustaafu na Baba Mtakatifu kuridhia Oktoba Mosi, mwaka jana.

Taarifa za kanisa zinaonyesha kwamba Askofu Rwoma aliteuliwa na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II kuongoza jimbo Katoliki Singida Aprili 19, 1999 na Januari 15, 2015 Baba Mtakatifu Benedikto XVI alimteua kuongoza Jimbo la Bukoba aliloliongoza hadi Oktoba, mwaka jana.

Askofu Rwoma alitumika kama Padre kwa miaka 48 na uaskofu miaka 23. Kwa mujibu wa TEC, Askofu Mteule Kyando alizaliwa Machi 7, 1964 Makete mkoani Njombe na alipata daraja la upadre Juni 19, 1996 jimboni Njombe.

"Amehudumu katika nafasi mbalimbali za utume jimboni Njombe na nje ya jimbo. Hadi uteuzi wake, Askofu Mteule alikuwa msaidizi wa Msimamizi wa Kitume Jimbo Katoliki Njombe," ilisema sehemu ya taarifa ya TEC.

Kuhusu Askofu mteule Mwijage, taarifa hiyo ya Padre Kitima ilisema alipata daraja la upadre Juni 20, 1997 jimboni Bukoba ambako amehudumu katika nafasi mbalimbali za utume jimboni humo. Taarifa ilifafanua kuwa Askofu Mteule Mwijage amewahi kuhudumu TEC kama Mkurugenzi wa Mashirika ya Kipapa.

Kabla ya uteuzi wa Askofu Mwijage, jimbo la Bukoba lilikuwa chini ya uangalizi wa Askofu Msaidizi Methodius Kilaini.

## 62 wanusurika ajali ya treni

**Na Christina Mwakangale**

WATU 62 wamenusurika kwenye ajali ya treni maarufu 'Treni ya Mwakyembe' huku wawili kati yao wakijeruhiwa vibaya.

Taarifa ya kuaminika iliyoifikia Nipashe juzi, ilisema ajali hiyo ilitokea eneo la Pugu, jijini Dar es Salaam, majira ya jioni na baadhi ya majeruhi kufikishwa Hospitali ya Rufani ya Amana, uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha ajali hiyo ni treni hizo mbili kuruhusiwa kimakosa kwenye njia moja na wakati mmoja.

Safari za abiria zimesitishwa hadi Jumatatu, wiki ijayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA), Conrad Simuchile, alisema ajali hiyo ilihusisha treni mbili, ya mizigo na abiria ambayo hufanya safari zake kati ya Tazara-Pugu Stesheni.

"TAZARA inasikita kutangaza kutokea kwa ajali iliyohusisha treni ya mizigo na abiria, Oktoba 17, mwaka huu, baada ya treni ya mizigo kugongana na ya abiria. Ajali ilisababisha majeruhi 62.

"Kati ya 62 wawili walikuwa na majeraha makubwa na kubaki hospitalini kwa matibabu zaidi na wengine waliruhusiwa kurejea majumbani," alisema Simuchile.

Pia, alifafanua kwamba uchunguzi wa awali kuhusu chanzo cha ajali hiyo, umebaini kwamba treni hizo mbili, ya mizigo na abiria, ziliruhusiwa kimakosa kwenye njia moja na muda huo huo.

"Ajali ilitokea wakati treni mbili ziliruhusiwa kimakosa kwenye njia ile ile inayotumiwa na treni ya umma na treni ya mizigo iliyobeba shaba," alisema Simuchile.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika jukwaa la tatu la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Italia, lililofanyika Milan, Italia jana. **PICHA: OWM**

# PM anadi vivutio uwekezaji Italia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara wa Italia kuwekeza Tanzania katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Amesema Tanzania ina malighafi za kutosha pamoja na uwapo wa masoko ya uhakika kutokana na eneo la kijiografia.

Majaliwa alisema hayo jana wakati akizungumza katika Jukwaa la Tatu la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Italia lililofanyika Palazzo Regione Lombardia, Milan nchini Italia.

Waziri Mkuu yuko nchini Italia akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Jukwaa la Kimataifa la Chakula Duniani ulioanza Oktoba 16, mwaka huu na unatarajia kufikia tamati leo, Rome nchini Italia.

"Msisitizo wa Mheshimiwa Rais Samia na mkakati wa serikali ni kuwahamasisha wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa mbalimbali Tanzania waje kuwekeza katika ujenzi na kuzalisha bidhaa hizo ili zipatikane kwa wingi na kwa urahisi," alisema Majaliwa katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyopatikana jana Dar es Salaam.

Majaliwa alitaja baadhi ya maeneo ambayo wawekezaji wanaweza kuwekeza ni katika sekta za madini, kilimo, mawasiliano, mifugo, uvuvi, utalii na afya. Alikaribisha wafanyabiashara hao na wawekezaji watumie fursa hiyo ya kuwekeza nchini.

Aidha, Waziri Mkuu alisema licha ya Tanzania kuwa na maeneo na mazingira mazuri ya uwekezaji, pia ina vivutio vingi vya utalii, hivyo alizikaribisha kampuni na mawakala wa utalii kuwekeza katika ujenzi wa hoteli za kitalii katika miji mbalimbali yakiwamo majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, barabara, viwanja vya ndege na nishati ya uhakika ili kurahisisha shughuli mbalimbali zikiwemo za uwekezaji.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Italia, Mahmoud Thabit Kombo, alitumia fursa hiyo kuwahakikishia ushirikiano wawekezaji na wafanyabiashara wote kutoka Italia ambao watahitaji kuwekeza na kufanya biashara nchini.

Jukwaa la Tatu la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Italia limehudhuriwa na zaidi ya wafanyabiashara na wawekezaji 300 kutoka mataifa hayo. Mbali na wafanyabiashara na wawekezaji, pia limehudhuriwa na wakurugenzi na wakuu wa taasisi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Baadhi ya taasisi hizo ni Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Kukuza ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA). Viongozi wa taasisi hizo walipata nafasi ya kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko nchini na namna ya kuwawezesha kuyafikia maeneo hayo.

# Wakazi Magomeni Kota walia na kero ya bili ya maji

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wakazi wa Magomeni Kota, wanaoishi kwenye kaya 644 wameelezea kero wanazokumbana nazo, zikiwamo ukosefu wa huduma muhimu za kijamii kama ukosefu wa huduma ya maji safi.

Hali hiyo inatokana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kusitisha huduma baada ya deni kuwa kubwa.

Wamesema hatua ya kusitishiwa huduma hiyo inatokana na miongoni mwao kugomea kulipia gharama ya huduma (service charge), wakidai kiwango wanacholipia kila mwezi cha Sh. 30,000 kwa kila kaya hakifikishwi kwa mtoa huduma.

Chanzo cha kuaminika kiliiambia Nipashe jana kwamba notisi ya kusitishiwa huduma kutoka DAWASA iliyoambatana na bili, inaonyesha wakazi hao wanadaiwa Sh. 6,617,308 ikiwa ni malimbikizo kuanzia Januari, mwaka huu, na hadi mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu, deni likisalia Sh. 3,970,308.

Mmoja wa wakazi katika makazi hayo, Mwajuma Hamisi (84), alisema kwa miezi mitatu hawana maji safi na kwa umri wake inamuwia vigumu, huku akitegemea wajukuu zake wamtafutie kutoka kwenye visima vya maji.

"Maji ukikosa ni tatizo kubwa na tunatumia ya kisima tulichimbiwa na mbunge wetu mwaka jana mara baada ya kuhamia na kinatusaidia kwenda kuteka huko. Mimi miguu sina natembelea baiskeli maalum. Miezi mitatu hatuna maji," alisema.

Hamisi alisema wakazi hao baadhi hawalipii gharama ya huduma, huku wachache ndio waliokuwa tayari kulipia na kusababisha huduma kusitishwa.

"Maghorofa matano tumewekewa mita moja kweli? Wakazi katika kaya 644 na kila kaya na matumizi yake. Tunaolipa wachache, wengine wamegoma wanasema kila mmoja awe na mita yake, apokee bili yake, tusibebeane mizigo," alisema.

Mwenyekiti wa wakazi hao, George Abel, alisema kusitishwa kwa huduma hiyo kunatokana na malimbikizo ya deni kuanzia Januari mwaka huu, hivyo utaratibu uliopo ni kulipa kwa awamu na kwamba kati ya Sh. 6,617,308 zilizosalia ni Sh. 3,970,308.

Meneja Uhusiano wa DAWASA, Everlasting Lyaro, alisema: "Hilo suala ni kweli na kuna jambo linaendelea, wiki iliyopita Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni alifanya kikao baina yake na wawakilishi wa wakazi, DAWASA.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Bernard Mayemba, alisema: "Wanufaika wanakatiwa maji kutokana na kutolipa bili. Wakala uliendelea kulipia huduma kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka jana, na mradi ulipozinduliwa Machi, 2022 wakazi walipewa ofa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati akizindua makazi kwamba kwa miezi mitatu wasilipie huduma wakati wanajipanga.

"Wakala ndiyo ni mmiliki ila anawajibika kushugulikia changamoto kama vitasa, miundombinu mingine kwa kipindi cha miaka mitano. Mei, mwaka huu, DAWASA walituandikia barua TBA kwamba tulipe bili ya maji ambayo ilikuwa takribani Sh. milioni 25.

"Bajeti tuliyokuwa nayo kila jengo na mnufaika awe na mita yake, ikafanyika tathmini ili tujue tutaweza kufanya hivyo au la kwamba kila kaya iwe na mita. Ila uwezo wetu ulikuwa kila jengo liwe na mita moja ambamo kila jengo kuna wakazi kuanzia 128 hadi 144," alisema.

Mayemba alisema kiutaratibu, TBA haihusiki katika kulipia huduma za kijamii kama vile maji na maji taka, uondoshaji taka, na kwamba makubaliano ni kushughulikia gharama za kiufundi za miundombinu kwenye maghorofa hayo.



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akizungumza na viongozi mbalimbali wa serikali wahusika wa sekta ya mazingira katika kikao kazi maalum, jijini Dodoma jana.**PICHA:OMR**

# Balozi ataja mafanikio ziara ya Samia India

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa India nchini, Pradhan Binaya (pichani), ametaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kupitia ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini India huku akisema kuwa, wawekezaji wengi wameonyesha nia kuja Tanzania kuwekeza sekta ya afya na elimu.

Katika mkutano na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Balozi Binaya, aliainisha faida ya ziara hiyo katika sekta mbalimbali za uwekezaji, kilimo, afya, elimu na maji na wawekezaji nchini humo, wakimwomba Rais Samia kuwatafutia maeneo ya kuwekeza.

Balozi Binaya alitaja mafanikio mengine ya ziara hiyo kuwa yamelenga kukuza biashara kati ya nchi hizo na kuvuka kiwango cha mauzo.

Pia alibainisha kuwa, hakuna nchi inayoweza kushindana na Tanzania katika suala la mauzo ya parachichi kwenda India.

Vilevile, alisema mafanikio mengine ni kutiwa saini kwa hati za makubaliano mbalimbali katika sekta tofauti za serikali na za binafsi, wakati wa kongamano la biashara, ikiwamo sekta ya utamaduni na michezo.



"Tanzania inaiona India kama soko kuu la parachichi. Pia India na Tanzania kushirikiana katika maeneo yenye maslahi kwa pamoja, ikiwa ni pamoja na biashara ya zao la parachichi," alibainisha.

Balozi huyo alikumbusha kuwa, Tanzania na India zilitiliana saini mikataba katika sekta mbalimbali, ikiwamo huduma ya afya, elimu na ushirikiano wa baharini, huku wawekezaji wa India wakionyesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo.

Vilevile, alisema Rais Samia aliangazia uwezekano wa kuongezeka kwa biashara kati ya India na Tanzania, ikilenga kuvuka kiwango cha mauzo cha Dola za Marekani bilioni saba.

"Waziri Mkuu wa India na Rais wa Tanzania walifanya mashauriano ya kina, yakijumuisha masuala mbalimbali yakiwamo changamoto za nchi mbili, kikanda, kimataifa na kimaendeleo.

"Viongozi hao wawili walishiriki chakula cha mchana akiwamo Waziri Mkuu nchini India na katika vyakula vilivyoandaliwa lilikuwamo parachichi kutoka Tanzania, na viongozi wote wawili walifurahia wanamuziki wa India wakicheza muziki wa Tanzania," alisema.

Kadhalika, alikumbusha Rais Samia alivyotunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa (Doctorate Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru, akiangazia uongozi wake na mchango wake katika uhusiano wa India na Tanzania.

Balozi Binaya alisema Tanzania na India zimekuwa zikiinua uhusiano wao kwa ushirikiano wa kimkakati, na ufadhili wa masomo.

# Mvua yenye upepo yasababisha maafa

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MTU mmoja amefariki dunia kutokona na mvua iliyoambatana na upepo mkali katika kata za Rwamishenye, Kashai na Hamgembe wilayani Bukoba huku nyumba 105 zikiharibiwa.

Madhara ya mvua hiyo iliyonyesha usiku wa kuamkia jana, yanaelezwa kuwa makubwa kwa wakazi hao na yamesababisha watu kuhama makazi huku juhudi mbalimbali za kuwasaidia zikifanyika.

Akizungumzia tukio hilo jana, Diwani wa Rwamishenye, Sued Kagasheki, alisema alianza kupokea simu za watu wakihitaji msaada kuanzia saa 10:00 usiku wa kuamkia jana akiwa nyumbani kwake.

"Tukachukua jukumu la kuanza kufanya tathimini kwa kushirikiana na watendaji na wenyeviti wa mitaa lakini hali haikuwa nzuri kabisa. Nyumba nyingi zilikuwa zimebomoka na kuharibiwa vibaya," alisema Kagasheki.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, alisema hatua za kusaidia familia zilizoathiriwa na mvua hiyo zimeanza ili kutoa misaada mbalimbali kwa waathirika hao.

Sima alisema, usiku wa kuamkia jana tukio hilo lilipotokea, alipokea simu za wadau mbalimbali waliohitaji kusaidia familia kwa kutoa vifaa mbalimbali vikiwamo shuka na blanketi.

Alisema ofisi ya maafa ya wilaya inaendelea kupokea taarifa kutoka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuangalia idadi kamili ya kaya zilizoathiriwa.

"Baadhi ya waathirika wa mvua hizi tumewatafutia maeneo ya kukaa na wengi ilionekana wameenda kwa jamaa na ndugu zao. Bado tunaendelea kupokea taarifa kutoka kwenye maeneo yaliathiriwa na ziko timu ngazi ya kata zitasaidia wale wadau wanaotaka kutoa misaada kujua idadi "alisema Sima.

Pia alisema nyumba 106 zimethibitika kuharibika zikiwamo 74 zilizoezuliwa mapaa ambazo zinaweza kurekebishwa lakini 72 zimebomolewa na kuezuliwa na zinatakiwak ujengwa upya.

Alisema kwenye idadi ya nyumba hizo, kuna majengo ya taasisi za serikali na kanisa ambayo ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri inafanya tathmini ya jinsi gani ya kurejesha mapaa yaliyoezuliwa.

Padri Egidius Rweyemamu wa Kanisa Katoliki Parokia ya Rwamishenye, alisema majira ya asubuhi akiwa kanisani akisali na waumini, watatu kati yao walijeruhiwa na kupelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, mjini Bukoba kwa ajili ya matibabu.

Alisema tangu kutokae kwa tukio hilo hadi sasa, uongozi wa kanisa unafanya tathmini kuangalia jinsi ya kurejesha paa la kanisa lililoezuliwa na upepo mkali.

# Muunganiko Tanga Cement, Twiga ulivyobatilishwa

**Na Waandishi Wetu**

NI vuta nikuvute. Ndivyo inavyoonekana katika sakata la muunganiko wa kampuni ya Saruji ya Tanga na kampuni ya Scancem International DA baada ya Baraza la Ushindani la Kibiashara (FCT) kubatilisha uamuzi wa Tume ya Ushindani (FCC) ulioruhusu mchakato huo.

Uamuzi huo ni tofauti na uliotolewa Julai 6, mwaka huu, ambao wajumbe watatu wa FCT walikinzana kuhusu Kampuni ya Saruji ya Chalinze kuhusu kulalamikia muunganiko huo Katika uamuzi wa Julai, Mwenyekiti wa FCT, Jaji Salma Maghimbi, alikubali uhalali wa Chalinze kuwa mdaawa lakini wajumbe, Dk. Godwill Wanga na Dk. Onesmo Kyauke, walipinga kutokana na kufutiwa usajili na Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA).

Katika uamuzi mpya uliotolewa Oktoba 16, mwaka huu, kutokana na rufani iliyowasilishwa na Peter Heller, wajumbe wote wamekubaliana na kubatilisha uamuzi wa FCC kuhusu muunganiko huo wakisema una athari za kibiashara na unaweza kusababisha ukiritimba katika soko la saruji.

Awali, FCT ilitoa hukumu Septemba 23, 2022 kubatilisha na kutengua uamuzi wa FCC wa Aprili 6, 2022 wa kuidhinisha muunganiko wa masharti wa Scancem International DA inayomiliki kampuni ya Saruji ya Twiga katika umiliki wa Tanga Cement.

Baada ya uamuzi huo, Februari 28, 2022, FCC iliidhinisha upatikanaji wa asilimia 68.33 ya hisa za Tanga Cement huku ikidai kuwa mazingira ya soko yalibadilika jambo ambalo lilipingwa na wadaawa kuwa hakuna utafiti uliofanyika na pia kuhoji uharaka wa kufanya hivyo bila kushirikisha wadaawa katika tasnia ya saruji.

Hatua hiyo ya muunganiko huo, ilipingwa na Heller aliyewasilisha ombi FCT. Wajibu rufani katika shauri hilo Na. 7 la mwaka 2023, lililowasilishwa na Heller ni FCC, Scancem International DA, Fayaz Bojohan, William Erio na Hakan Gurdan.

Baada ya mawakili wa pande zote kuwasilisha hoja mbele ya jopo la wajumbe wa FCT, iliamuliwa kuwa uamuzi wa awali uliotolewa kwa ukinzani baina yao, umebatilishwa na kusisitiza kwamba muunganiko huo ni batili.

Kutokana na kukuibaliana huo, jopo hilo lilibainisha kwamba: "Uamuzi wa washtakiwa (FCC) wa Februari 28, 2023 katika ombo la kuunganisha namba ya CBC. 127/359/144, unasomeka uamuzi wa Oktoba 16, 2023 ulitolewa na Jaji Salma Maghimbi (Mwenyekiti wa FCT), Dk. Onesmo Kyauke (mjumbe) na Godwill Wanga (mjumbe)."

Katika uamuzi huo, FCT pia ilisema imezingatia ma kukubali ushauri wa Wakili Mkuu wa Serikali, Deodatus Nyoni, aliyaiwakilisha FCC kwamba mahakama ibatilishe uamuzi wa FCC wa Februari 28, 2023 katika muunganiko huo na kuruhusu walalamikiwa kutuma maombi ya mapitio ya uamuzi wa baraza wa Septemba 23, 2022. Uamuzi huo ulitamka kuwa muunganiko huo haukuwa halali na kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu katika mchakato mzima.

"Kwa maoni yetu, kupitishwa kwa ushauri mzuri wa Nyoni unaomumiza, usipiosikilizwa kutatutenganisha katika mzozo huu," ilibainisha sehemu ya uamuzi huo wa jopo la wajumbe wa FCT.

Katika hukumu yake hiyo pia, FCT ilisema haikuwa nia yake ya kusababisha usumbugfu na ucheleweshaji usio wa lazima kwa wawekezaji. Uilisema inafanya kazi yake ya usimamizi wa ushindani na mamlaka yake ya udhibiti katika kutekeleza madhumuni ya Sheria ya Ushindani (FCA) ambayo ni kulinda na kukuza ushindani thabiti katika biashara ili kuwalinda watumiaji dhidi ya mwenendo wa soko wa haki na udanganyifu na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Aidha, FCT ilisema kwa kuzingatia hilo, inafanya uamuzi unaoendana na sera za serikali ambazo zinalenga kuvutia na kuhifadhi uwekezaji wa moja kwa moja wa ndani nan je ya nchi na kuondoa mitazamo ya urasimu inayokatisha tamaa wawekezaji muhimu.

HABARI KITAIFA

# Kanzidata ya taarifa za viwanda kuandaliwa

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), limesema linaandaa kanzidata ya taarifa za viwanda vyote vilivyopo nchini na kuziweka kwenye mfumo maalumu utakaorahisisha upatikanaji rahisi wa taarifa hizo kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje.

Akizungumza na Nipashe jana, jijini Dar es Salaam Mkurugenzi wa TEHAMA na Maendeleo ya Teknolojia TIRDO, Masoud Masoud, alisema litahusisha ukusanyaji wa taarifa mbalimbali zikiwamo kuonyesha kila kiwanda kikowapi, katika mazingira gani, na kinatumia malighafi gani na zinapatikana wapi, pamoja na upatikanaji wa miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano.

Alisema kanzidata hiyo itaonyesha pia hali halisi ya idadi ya rasilimali watu katika viwanda, na kwamba lengo ni kuhakikisha kila kiwanda kinakuwa na taarifa sahihi na moja yenye uthibitisho, akisema kuwa wawekezaji wanahitaji kupata taarifa kamili za eneo wanapohitaji kwenda kuwekeza.

"Baada ya kuzikusanya hizi taarifa na ili kuweka uwezekano wa kila mtu kuzifikia tutakuwa na kanzidata, baada ya hapo watu wote na taarifa zote nchi nzima zinazohusu viwanda na uwekezaji atakuwa anazipata kupitia data base hiyo kwa uhakika," alisema na kuongeza:

"Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani viwanda vingi viko chini ya asilimia 50 ya 'capacity' (uwezo) ya uzalishaji kwa sasa na ile 'maximum capacity' ya mitambo inayotakiwa kuzalisha, sasa hii inamaanisha kwamba tungejua sababu zinazosababisha kuzalisha chini ya uwezo ni rahisi serikali kujikita kuangalia jinsi gani ya kuongeza uzalishaji," alisema Masoud. Alisema kuwa kanzidata hiyo itaonyesha pia ni bidhaa gani zinazozalishwa na viwanda Tanzania, wangapi wanataaluma na wasiokuwa na taaluma, wanawake, wanaume, idadi ya watanzania na wasio watanzania.

Pia alibainisha kuwa eneo lingine litaonyesha taarifa za uwekezaji, kama maeneo ya mauzo, eneo gani linafaa kwa uwekezaji gani na ni rasilimali gani itafaa kuwekeza katika eneo husika, viwanda vina uwezo kiasi gani na sasa hivi vinatakiwa kuzalisha kwa asilimia ngapi.

Alisema itaonyesha pia kwamba kiwanda kina leseni au hakina, kinatoa wapi na mamlaka yake ni ipi inayotoa leseni, ikiwamo kuonyesha vilivyopatiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

"Itaonyesha pia zinapopatikana huduma za 'technical' kwenye viwanda, wafike hapa ndiyo sehemu tunawasiliana na wenye viwanda, kutapatikana taarifa za maghala yako mangapi, wapi, yanafanya nini, yanaukubwa kiasi gani na yanahifadhi vitu gani.

"Kutakuwa pia na eneo linaloonyesha ni viwanda gani vimekidhi vigezo vya uhalali wa kuwapo nchini, kwasababu kuna ambavyo vipo, lakini havijakidhi vigezo, na ili ukidhi unatakiwa kuwa na vitu gani, pia tutawawekea taarifa ya benki zinazoweza kuwapatia mikopo wenye viwanda ili iweze kuwasaidia kuendeleza uzalishaji," alisema Masoud.

Hata hivyo, alieleza kuwa mtu yeyote atakaehitaji kuanzisha kiwanda atalazimika kwenda kusajiliwa kwenye mfumo huo ili taarifa zake zipatikane.

# Wasafiri wanaokwenda Falme Kiarabu kufanya ununuzi kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu ya Airtel kwa ushirikiano na TerraPay, mtandao wa malipo bila mipaka, wamezindua huduma ya kufanya malipo kidijitali kimataifa inayowezesha wateja wa Airtel Money wakiwa nchi za Falme za Kiarabu (UAE) kufanya ununuzi kwenye vituo vya mauzo kwa kutumia akaunti zao za Airtel Money bila gharama ya ziada.

Hii inafuata baada ya Airtel Tanzania kupitia huduma ya Airtel Money kutangaza punguzo katika ununuzi wa tiketi za ndege za Fly Dubai kwa punguzo la asilimia 10 kuanzia mwezi Julai.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa kutangaza ushirikiano huo mpya, Mkurugenzi wa Airtel Money, Andrew Rugamba alisema: "Airtel Tanzania imejizatiti kutoa huduma zenye masuluhisho zaidi kulingana na mahitaji ya kila siku ya wateja wetu tukizingatia thamani zaidi kwa wateja.

Ubia wetu Airtel Money na TerraPay, tunalenga kutatua changamoto za malipo ambazo wateja wetu wanakutana nazo wanaposafiri kwenda nchi za Falme za Kiarabu. Tunatambua sera makini za serikali za kujenga ushirikiano kimataifa ambazo zimekuwa zikijenga mahusiano mazuri ya biashara na nchi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na UAE.

Idadi inayoongezeka ya wasafiri wa Kitanzania wanaotembelea Falme za Kiarabu kwa madhumuni mbalimbali, kama vile biashara, utalii, ziara rasmi, na shughuli za serikali, inaonyesha ongezeko la uhitaji. Ushirikiano wetu na TerraPay unaondoa haja ya wasafiri kubeba fedha nyingi au kupitia usumbufu wa kubadilisha fedha kila wanapokwenda UAE."

Ili kupata huduma za malipo ya nje ya nchi kupitia TerraPay, wateja wa Airtel Money wanatakiwa kutembelea eneo lolote la mfanyabiashara lenye nembo ya TerraPay nchini UAE. Mfanyabiashara atafanya muamala kwenye kituo malipo / POS. Mteja wa Airtel Money atapokea ujumbe wa kuingiza nambari yake ya siri na kuthibitisha muamala.

Mteja wa Airtel Money atapokea ujumbe wa kuthibitisha muamala utakapokamilika. Rugamba alisisitiza kuwa Airtel Money inaendelea na ubunifu wa kuzifanya huduma kuwa jumuishi kwa kuweka kila kitu pamoja kwa lengo la kutoa huduma za haraka, rahisi, salama na kwa gharama nafuu zaidi. Huduma nyingi zinazopatikana kupitia Airtel Money zitaiweka Airtel katika nafasi ya mtoa huduma bora anayekubalika.

Willie Kanyeki, Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika wa TerraPay, alizungumzia umuhimu wa ushirikiano wao na Airtel Money kuwa ni mkakati unaolenga kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wateja wakiwa popote kwa kuhamasisha shughuli za kiuchumi kufanyika kidijitali.

"Ushirikiano wa Airtel Money na TerraPay unadhihirisha dhamira ya Airtel Money kuendelea kutoa huduma za kisasa kwa wateja wake. Wanaendelea kutoa bidhaa na huduma ambazo wateja watafurahia wakati wowote, wakiwa mahali popote, dhamira ambayo TerraPay inaishi kwayo."


eastafrica RADIO
EATV

East Africa Television Ltd
P.O. BOX 4374, Mikocheni Light Industrial Area,
Dar es Salaam, Tanzania, East Africa.
Tel: + 255 (22) 2775914/6
Fax: +255 (22) 2772752
Email:info@eatv.tv

## CAREER OPPORTUNITIES

**EAST AFRICA TELEVISION LTD,** the number one youth channel that has grown to a regional with vigor content of educating and entertaining programs. **EATV** is looking for suitable and qualified people to fill in the following vacancies:

**JOB TITLE** : **PRODUCER (NEWS & CURRENT AFFAIRS)**
**Job purpose** : Conceptualize, plan, develop, coordinate and execute (LIVE OR RECORDED) program/s to achieve maximum viewer interest, audience following, ad-sales profits and rating results.

As a news producer, you will oversee the editorial content of the news, collaborating with news editors, reporters, and anchors, while also supervising the overall content and flow of news distribution to the public.

**Responsibilities**

- Gather information, stories and pieces from team members throughout the day and Produce content for TV, Radio and Digital platforms
- Collaborate with Head to select and prioritize content
- Add creative elements that will make the broadcast more attractive
- Select footage and sound bites to include in broadcast to ensure consistency
- Liaise with the production team to keep technical standards high
- Communicate with the studio crew and anchors while on-air and ensure broadcast is within time limits
- Produce breaking news reports
- Conduct marketing and promotional activities for the program while liaising with marketing section for needs and requirements.
- Perform research on local, national and international affairs to stay updated with current events
- Meet the periodical performance set target
- Perform any other related duties as assigned.

**Skills:**
Excellent Communication Skills, fluent in English and Kiswahili

**Qualification:**

- Diploma in TV Production, Mass communication/Journalism
- Two years working experience as Producer
- Excellent Leadership, organizational and time management skills
- Solid experience with digital technology

Interested candidates who meet the above criteria should send in their applications enclosing a detailed CV addressed to the:

**HUMAN RESOURCES DEPARTMENT**
**EAST AFRICA TELEVISION LTD**
**P.O.BOX 4374**
**DAR ES SALAAM – TANZANIA**
**Or by Email address: jobs@eatv.tv**

***Deadline 27th October 2023, Shortlisted candidates will be notified.***

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kupanda kwa nauli kuzingatie hali za maisha ya Watanzania

**WAMILIKI** wa mabasi ya abiria ya kwenda mikoani na nje ya nchi na yale ya daladala mkoani Dar es Salaam, wamewasilisha ombi katika Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuomba ongezeko la nauli kutokana na sababu mbalimbali. Wamiliki hao wamewasilisha ombi lao katika kikao kilichofanyika juzi baina yao na mamlaka hiyo kupitia Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) na Chama cha Wasafirishaji Mkoa wa Dar es Salaam (DARCOBOA).

Katika ombi lao hilo, wamiliki hao wanataka kupandishwa kwa viwango ya nauli za mabasi ya mikoani na yale ya daladala kwa viwango tofauti sababu kubwa ikiwa ni kupanda kwa mafuta. Wamebainisha kuwa ndani ya miezi mitatu, lita moja ya mafuta imepanda kwa wastani wa Sh. 1,000.

Sababu nyingine waliyoitoa ni gharama za uendeshaji zikiwamo ununuzi wa vifaa na kupanda kwa Dola ya Marekani ambayo hutumika kwa ajili ya uagizaji wa spea na vifaa vingine.

Wamikili wa daladala, kwa mfano, wametaka nauli inayotozwa Sh. 500 iongezwe hadi kufikia Sh. 800 huku katika umbali wa kilomita 25 iwe Sh. 1,200 kilomita 20 Sh. 1,600 na kilomita 30 iwe Sh. 2,400.

Baada ya kuwasilisha mapendekezo hayo, uongozi wa LATRA ulisema umeyapokea na utawasilisha mbele ya bodi ya wakurugenzi kisha wizara kwa hatua za utekelezaji na hatimaye kutoa majibu. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ambaye alihudhuria kikao hicho juzi, alisema sababu zilizotolewa na wamiliki hao ni za msingi lakini akashauri LATRA kuyafanyia kazi mambo hayo bila kuwaumiza wananchi.

Kwa ujumla, sababu zilizotolewa na wamiliki wa mabasi ni za msingi na zinapaswa kufanyiwa kazi. Ni ukweli ulio wazi kwamba bei za mafuta kwa kipindi kifupi zimekuwa zikipanda kila mwezi jambo ambalo lina athari kubwa katika uendeshaji wa masuala mbalimbali ya shughuli za maendeleo, usafirishaji ukiwamo.

Ni dhahiri kwamba kuongezeka kwa bei za mafuta mara kwa mara na kupanda kwa Dola, sarafu ambayo inatumika katika ununuzi na miamala ya biashara kimataifa ikiwamo uagizaji wa mafuta na vipuri vya magari vinawazidishia mzigo wamiliki wa magari yakiwamo yale ya abiria - mikoani na katika miji, maarufu kama daladala.

Kutokana na hali hiyo, ni wazi kwamba kupanda kwa gharama hizo kunawafanya wamiliki kubeba mzigo wa ziara katika kutekeleza majukumu yao na matokeo yake ni kupata hasara katika biashara zao. Kanuni kubwa ya biashara ni kumwezesha mfanyabiashara au mtoa huduma yeyote kupata faida na si hasara. Kwa mantiki hiyo, hoja ya wamiliki wa vyombo vya usafiri ni ya msingi na inapaswa kufikiriwa kwa mtazamo chanya ili kuwapunguzia makali.

Pamoja na ukweli huo, ni vyema pia wasafirishaji wakatambua kwamba kama alivyosema mwanafalsafa mashuhuri wa India, Mahatma Gandhi, wapiganapo tembo hata wafanyapo mapenzi, ni nyasi ndizo ziumiazo, hivyo hivyo jambo lolote la nyongeza ya nauli au bei ya bidhaa linapofanyika, mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi ndiye aumiaye.

Kwa mantiki hiyo, suala la kufikiria kupandishwa kwa nauli kama lilivyoombwa na wamiliki, lizingatie kuwapa unafuu kwa kiasi fulani wananchi ambao ndio wanaobeba mzigo wa gharama hizo. Iwapo gharama zitakuwa kubwa wananchi wengi watashindwa kuzimudu na matokeo yake wataingia katika umaskini.

Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba kupanda kwa nauli, kunakotokana na sababu zilizoainishwa na wasafirishaji, zina athari za moja kwa moja katika kuongeza gharama za maisha, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuwaonea huruma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# TEHAMA, nguzo iliyosahaulika kwenye vipaumbele mikopo mipya vyuo vya kati

Na Christina Mwakangale

**NIKADIRIE** wastani wa wiki mbili hivi zimepita, serikali ilitangaza vipaumbele vipya kwenye elimu kwa kupatiwa mikopo hususan maeneo sita, kwa wanafunzi wa stashahada (diploma), ikitenga Sh. bil 48 kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi 8,000 watakaofanyiwa udahili katika mwaka wa masomo 2023/24.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, mnamo Oktoba 4 mwaka huu, akizindua Mwongozo wa Utoaji Mikopo ya Elimu kwa Wanafunzi wa Stashahada, akiwa mkoani Dar es Salaam anasema uamuzi huo ni marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) wa mwaka 2017.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa bodi hiyo kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada nchini.

Ikumbukwe, huo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Dk. Samia Samia Suluhu Hassan, kutaka wanafunzi wa vyuo vya kati kunufaika na mikopo ya serikali, ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya Afrika kuhusu rasilimali watu.

Mikopo hiyo ipo katika vipaumbele sita na mahsusi kwa wanaosoma; Afya na Sayansi Shirikishi; Elimu (stashahada ya ualimu wa masomo ya Fizikia, Hisabati na amali; Usafiri na Usafirishaji); Uhandisi wa Nishati; Madini na Sayansi ya Ardhi; Kilimo na Mifugo.

Mbali na vipaumbele hivyo, binafsi naona wazi serikali imesahau eneo muhimu kupatiwa mikopo, Stashahada ya Teknolojia ya Habari Mawasiliano (TEHAMA), ambayo ndio msingi na tegemeo kwenye sekta zote nchini, afya, kilimo, mifugo, fedha, maji, elimu, nishati na madini.

Hivi sasa ubunifu wote na uandaaji wa shughuli za maendeleo unawategemea wataalamu wa teknolojia. sekta ya Afya, ikiwa ni kipaumbele kimojawapo cha kupatiwa mkopo huo, ni miongoni ambazo kazi zake zinafanyika kwa asilimia 70 kwa msaada wa TEHAMA.

Vifaa vya kidigitali kuanzia vifaa vya X-Ray, CT scan, MRI na hata vipimo vidogo, enzi za kutumia muda mrefu kusubiri majibu ya vipimo kwa magonjwa tofauti imepitwa na wakati, kutokana na kukua kwa teknolojia.

Kadhalika, wagonjwa kuanzia ngazi ya chini hadi mkoa na rufani, hutegemea teknolojia na si ile ya zamani ya kumwandikisha mgonjwa kwa kutumia makaratasi, kalamu na mafaili kuweka masijala.Pia, matibabu hutumia tiba mtandao, kuna aina kadhaa za upasuaji na upangaji wa dawa kwa wafamasia wakitegemea teknolojia ya kompyuta kwa kutunza kumbukumbu kujua iwapo dawa fulani ipo stoo au la, na inaweza kupatikana wapi, si kama awali ilihitaji mtu azame stoo kupekua, ndipo ajue idadi ya dawa zilizopo.

Madaktari bingwa wanabadilishana uzoefu na wenzao walioko nchi za mbali, kwa kutumia teknolojia mtandaoni wakiunganisha skrini moja hapa (nchini) na wenzao, kumfanyia upasuaji mgonjwa bila ya kuhitaji kumsafirisha bingwa afike nchini ili kutoa usaidizi.

Kwa kutumia programu tumishi (application), mtandaoni huduma ya 'M-mama', imeleta faraja miongoni mwa kinamama, ikiokoa Maisha, sambamba na vifo kupungua.

'M-mama' ni programu ya teknolojia inayotumia simu ya mkononi kuwaunganisha wanawake wajawazito na huduma ya usafiri wa dharura walioko vijijini. Imekwishatoa huduma ya usafiri wa dharura kwa wajawazito 24,290 na watoto wachanga 4.822 huku zikifanywa safari 29,152 na kuokoa vifo takribani 1,000.

Juni 14, mwaka huu, Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), iliyopo jijini Dodoma, kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji Mfumo wa Mkojo Tanzania (TAUS), ilianzisha teknolojia mpya kwa kuwapandikiza wanaume wawili, visisimua uume (Semi Rigid Penile implantation) kwenye uume.

Kwenye elimu ndiko usiseme, kumebobea matumizi ya kiteknolojia hivi sasa kila kitu ni mtandaoni. Nani aliwahi kifikiri kwamba hata matokeo ya wanafunzi wa darasa la nne huko shule za msingi, majibu tutayapata mtandaoni?

Unapozungumzia fizikia, sayansi kuelekea kuwapata wahandisi kwenye sekta tofauti kama nishati, madini, maji tegemeo kuu ni teknolojia.

Michoro ya ramani za majengo ilitumia kalamu za risasi, karatasi likiloana na maji, mchoro kwaheri! Sasa ramani inatunzwa kidigitali.

Katika kilimo na mifugo, pia kumesheheni watafiti wa ngazi za juu wenye elimu ya PhD, ambao wanategemea teknolojia kufanya utafiti na kupata majibu ya haraka na inaweza kuunganisha 'spishi' moja na nyingine, ili kuboresha uzalishaji katika kilimo au mifugo.

## HABARI KITAIFA

# Pwani kinara uandikishaji wanafunzi darasa awali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKOA wa Pwani, umekuwa kinara wa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali kwa kuvuka lengo la serikali la asilimia 100 na kufanikiwa kuwasajili kwa asilimia 127 kwa mwaka huu.

Aidha mkoa wa Pwani, umefanikiwa wanafunzi wake kuanzia darasa la kwanza kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa asilimia 99 huku asilimia 93 ya wanafunzi wa darasa la tatu wakiwa na umahiri wa kujieleza kwa lugha ya Kiingereza.

Pia mkoa huo umekuwa wa mfano nchini kwa kufanikisha utoaji wa chakula shuleni kuanzia ngazi ya Msingi hadi Sekondari kwa asilimia 67.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu wazima na wale walio nje ya mfumo wa elimu yaliyofanyika kitaifa Mailimoja, Kibaha mkoani Pwani.

"Mkoa huo umefanya vizuri kwenye sekta ya elimu na kuhamasisha mikoa mingine kujifunza kutoka kwao ili kuisaidia serikali kuboresha upatikanaji wa elimu nchini," alisema Dk. Msonde.

Akizungumzia mafanikio hayo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliema kwa kushirikiana na watalaamu pamoja na walimu wa mkoa huo wanafanya kazi kwa njia ya ushirikishwaji na wameweka mikakati ya kuboresha elimu na kuongeza ufaulu.

Alisema kuwa kati ya shule 748 za msingi mkoani humo 632 zinatoa chakula shuleni na kati ya 219 za sekondari 137 chakula kinapatikana.

"Hii ni Pwani yetu imekuwa na mikakati mbalimbali kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye maeneo yote ukiangalia katika viwanda, afya na elimu matokeo mazuri yanaonekana ukiwamo na mpango huu ya elimu ya watu wazima msingi (MEMKWA) kwa mwaka 2022, walioingia ni 54, 416 kwenye program hiyo na mwaka 2023, wanufaika ni 57,000" alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo, alisema serikali imeanzisha vituo 405 vya elimu ya watu wazima nchini.

Na kwamba katika vituo hivyo watu wazima milioni 5.7 wamejiunga ili kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) na mwamko bado ni mdogo.

"Nawasihi wananchi wasiojua kusoma kuandika na kuhesabu kuchangamkia fursa hiyo kwa sababu wanafundishwa na ujuzi ambao utawasaidia kuendesha maisha yao," alisema Prof. Carolyne Nombo.

Alitoa wito kufunguliwa kwa programu ambazo zitahamasisha matumizi ya Tehama na ujasiriamali ili kushawishi watu wengi kujifunza.



Diwani wa Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Stephen Mushi (mwenye kofia), akiwa na Katibu wa CCM wa kata hiyo, Gamaliel Mhanga, Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Jiji hilo, Sije Libe (wa pili kushoto), wakipata maelezo kuhusu vyakula lishe kutoka kwa Ofisa Lishe wa Jiji, Flora Mgimba (kushoto), kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani katika viwanja vya Mnadani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa aipa heko NIT utafiti changamoto sekta ya uchukuzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amekipongeza Chuo cha Taifa cha Usafirishahji (NIT) kwa kutambua umuhimu wa utafiti katika masuala mbalimbali yakiwamo utatuzi wa changamotio katika sekta ya uchukuzi.

Mbarawa alitoa pongezi hizo juzi wakati akifungua Mkutano wa Kimataifa

Kuhusu Uchukuzi na Usafirishaji ulioandaliwa na chuo hicho jijini Dar es Salaam.

Alisema wadau kutoka sekta ya uchukuzi wanaweza kutumia mkutano huo kubadilishana uzoefu na matokeo ya utafiti huo ambao umefanywa na chuo hicho.

Prof. Mbarawa alisema utafiti una mchango mkubwa katika kuleta maendeleo endelevu na kuipongeza NIT kuwa na msingi wa kutambua hilo.

"Tunahitaji maamuzi ambayo yametokana na utafiti ili kuleta tija katika sekta ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na kuleta maendelea ya kiuchumi na kijamii nchini," ALISEMA.

Aliwataka washiriki wa kongamano hilo la kwanza la Kimataifa la Usafiri, Usafirishaji na Usimamizi kutumia jukwaa hilo kuanzisha ushirikiano utakaoleta matokeo chanya.

"Kama serikali, tunaahidi kuendelea kutoa msaada unaohitajika kwa NIT na wadau wengine katika sekta hii ili kuhakikisha tunafanya kazi kwa pamoja na kuboresha sekta ya uchukuzi.

"Naelewa hili linapaswa kuwa jukumu letu sote yaani serikali, sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) na washirika wa maendeleo. Nawahakikishi nitafanya kazi bila kuchoka na busara ili kutatua changamoto mbalimbali katika sekta hii kwa kushirikiana na wadau wote wakiwamo wanaoshiriki katika hafla ya leo," alisema.

Kutokana na kaulimbiu ya mkutano wa mwaka ambayo ni "Usimamizi wa Uhakika wa Usafiri na Usafirishaji kwa Uchumi Endelevu", Waziri alisema inaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 - 2025, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2030, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

"Kwa kweli inafurahisha kuona kwamba Mkutano huu ni jukwaa la kubadilishana maarifa na matokeo ya utafiti ili kuboresha sekta ya usafirishaji," alisema.

Waziri wa Uchukuzi aliendelea kusema kuwa Serikali inaunga mkono kufanyika kwa Mkutano huo na imesema uwe unufanyika kila mwaka ili kuboresha utendaji wa sekta ya usafiri.

"Nafurahi kusema kwamba NIT inakua kwa kasi na kaulimbiu ya Mkutano huu inahusiana moja kwa moja na maendeleo ya miradi ya kimkakati ya kitaifa katika sekta ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), Reli ya Kisasa (GR), Ujenzi wa Tanzanite, Daraja la Nyerere na Kingongo Busisi, uboreshaji wa bandari za kisasa, kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na ununuzi wa ndege za kisasa za abiria na mizigo.

"Miradi mingine ni ukarabati na ujenzi wa uwanja mpya wa ndege na uendelezaji wa Uchumi wa Bluu, Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani Tanga, Tanzania na Mradi wa Kituo cha Umeme wa Maji cha Julius Nyerere. Ninaamini kwamba kupitia mkutano huu wadau mbalimbali na washirika wa maendeleo watapata njia za mashirikiano ili kuhakikisha kwamba maazimio ya Mkutano yanachukuliwa kwa ajili ya utekelezaji," alisema.

aliitaka NIT kuzalisha rasilimali watu kwa ubora wa hali ya juu ambao wanaweza kusaidia miradi mikubwa ya serikali katika sekta ya uchukuzi.

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema mMkutano wa mwaka huu ni hatua muhimu katika kufikia malengo katika Mpango wetu Mkakati wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026. Alisema lengo letu ni kuifanya jukwaa la kikanda kwa jumuiya ya wanasayansi katika nyanja za usafiri na usimamizi.

Prof Manilwa alibainisha kuwa mkutano huo unawakutanisha wadau mbalimbali waliobobea katika sekta ya usafiri kutoka nchini Tanzania na duniani kote.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Kampuni kupunguza wafanyakazi 500 SGR

**Na Vitus Audax**

KAMPUNI ya Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Yapi Merkezi, inatarajia kupunguza wafanyakazi 525 baada ya kupata mapendekezo yatakayofikiwa kati yake na walengwa ambao sio wanachama wa Chama cha Wafanyakazi (TAMICO) kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kufungwa kwa kambi ya Manyoni na Nyahua pamoja na tishio la El-Nino.

Katika taarifa ya kampuni hiyo kwa wafanyakazi wa kituo cha Tabora Makutopora iliyotolewa Oktoba 16 ilieleza kuwa sababu za kupunguza wafanyakazi hao ni pamoja na kufungwa kwa kambi ya Manyoni na Nyahua na tishio la mvua kubwa juu ya wastani kama ilivyotangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA).

Yapi Merkezi ilitaja utekelezaji wa upunguzaji huo utafanyika baada ya mchakato wa mashauriano kati ya kampuni hiyo na wafanyakazi kukamilika kuanzia Oktoba 31, mwaka huu au kabla ya hapo.

Katika barua hiyo mwajiri alifafanua kufikia uamuzi hayo kwa kutokupenda na kutaja njia mbadala ambayo ni mapendekezo ya likizo isiyo na malipo ikitajwa kuwa na unafuu wa kulipiwa asilimia sita yote ya NHIF na asilimia 14.28 ya kima cha chini cha mishahara ndani ya kampuni kwa wote wa mkupuo mmoja suala ambalo halikuafikiwa na wafanyakazi hao.

Ilitaja waathirika wa hatua hiyo baada ya makubaliano na kupunguza kutaendelea hatua kwa tatu hadi kufikia wafanyakazi 525 huku uteuzi wa wafanyakazi hao ukitarajiwa kufuata kielelezo kama kilivyobainishwa katika sheria ya kazi.

"Ni kusudi la mwajiri kushauriana na wewe kwanza katika kipindi hiki kabla ya uamuzi wowote wote wa mwisho wa kuchukuliwa. Mwajiri atakuarifu kuhusu tarehe na muda wa mashauriano," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha taarifa hiyo ilisema mwajiri atatoa msaada wa barua ya kumbukumbu pamoja na cheti cha Utumishi pamoja na kuhakikisha Sheria ya Ajira na Mahusiano mema kazini inafutwa na mwajiri kwa kumjulisha rasmi kuhusu kupunguzwa kwa wafanyakazi.

Aidha, taarifa hiyo iliyotolewa na idara ya rasilimali watu ya Yapi Merkezi Insaat Ve Sanayi ili waalikwa kutoa uwasilishaji, kushiriki kupitia mwakilishi atakaye mchagua mfanyakazi katika kikao cha mashauriano majadiliano juu ya kusudio la kupunguza baadhi ya wafanyakazi hao.

Hivi karibuni, kampuni hiyo ililalamikiwa kwa ucheleweshaji wa malipo ya fedha za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) za wafanyakazi kwa miezi tisa huku Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akisema kasi ya ujenzi wa reli kipande cha Makutupora - Tabora chini ya kampuni hiyo upo nyuma kwa asilimia 10.

Hivi karibuni serikali ilieleza kuwa mkandarasi huyo hadai fedha zozote kwa kuwa mpaka kufikia mwezi juni 2023 serikali ilikuwa imelipa jumla ya Sh. trilioni 8.13 kwa YAPI Merkezi na malipo yake yamefanyika kwa kila kipande.

Ilieleza vipande hivyo kuwa ni Dar es Salaam-Morogoro hundi 60 zenye jumla ya Sh. trilioni 2.55, Morogoro-Makutupora hundi 59 sawa na Sh. trilioni 3.75, Makutupora-Tabora hundi 10 sawa na Sh. billioni 883.25, Tabora - Isaka hundi nne na malipo ya awali sawa na Sh. bilioni 951.6.



Baadhi ya wastaafu watarajiwa wa Jeshi la Polisi nchini, wakishiriki mafunzo ya kujiandaa kustaafu yaliyoandaliwa na Benki ya NMB, jijini Dodoma jana, kupitia kampeni yake ya huduma kwa wastaafu ijulikanayo kama "Hekima Plan". **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vyuo vyaonyeshwa mwarobaini tatizo la ajira

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO Vikuu na vile vya kati vimeshauriwa kufanyakazi kwa karibu na waajiri ili kuboresha mitaala itakayovisaidia kutoa wahitimu wanaofaa kwenye soko la ajira.

Ushirikiano huo umeelezwa utasaidia kuwapa wanafunzi fursa ya kufanya mafunzo ya vitendo, kupata uzoefu na kuondoa malalamiko kuwa wahitimu wengi hawaajiriki.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Udhibiti Ubora wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Gordian Bwemero, wakati akizungumza na wadau wa chuo hicho kuhusu proramu mpya ya uanagenzi waliyoanzisha.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa waajiri kwamba wahitimu wengi wa vyuo vikuu hawamudu vyema majukumu yao wanapoajiriwa moja kwa moja baada ya kuhitimu masomo yao.

Alisema tatizo la ajira kwa vijana duniani ni changamoto kubwa na zipo sababu mbalimbali zinazosababisha hali hiyo ikiwamo ukosefu wa fursa za ajira ambazo ni chache kulinganisha na wanaohitimu

"Tunashuhudia ongezeko kubwa la wahitimu kila mwaka na kwa Tanzania inakadiriwa kwa mwaka wastani wa wanafunzi 800,000 mpaka 1,000,000 wanahitimu, lakini kati ya hao ni asilimia 5.7 ndio hufanikiwa kupata ajira kwenye sekta rasmi," alisema.

Bwemero alitaja jambo lingine kuwa ni tatizo la ukosefu wa sifa zinazohitajika kwenye soko la ajira kwa kuwa wengi wanakosa ujuzi na uzoefu na katika utafiti mbalimbali waajiri wanalalamikia kuwa wahitimu wengi hawana ujuzi.

Bwemero alisema baadhi ya watu wanawalaumu vijana kushindwa kujituma kutafuta ujuzi na utaalamu unaohitajika sokoni wakiwa vyuoni na wengi wao wanapokuwa vyuoni wanasoma ili wafaulu mitihani.

Alisema baadhi ya watu wanailaumu serikali kwa kutoweka mazingira mazuri, sera, na mikakati bora ya kutoa fursa za ajira kwa vijana wakati wengine wanasema sekta binafsi haijawekeza vya kutosha kutengeneza fursa za ajira kwa vijana.

Aidha, alisema baadhi ya watu wamekuwa wakilaumu vyuo vikuu na vya kati kwa kushindwa kuzalisha wahitimu ambao wana ujuzi stahili unalohitajika kwenye soko la ajira.

"Kwa mfano wanasema elimu ya nadharia imepewa kipaumbele sana kwa ufundishaji na upimaji wa wanafunzi vyuo vingi vimejikita sana kwenye nadharia kuliko vitendo na wanasema mafunzo yanayotolewa vyuoni hayaendani na mahitaji ya kwenye soko la ajira," alisema.

Alisema katika jitihada za kupunguza tatizo la ajira vyuo vikuu na vya kati vinatakiwa kutoa elimu ya ujasiriamali ili kutoa wahitimu wabunifu wanaoweza kutengeneza fursa za ajira kwao wenyewe na kwa wengine.

Alivishauri vyuo kuanzisha mafunzo ya uanagenzi ambayo yatawawezesha wahitimu wao kuwa na ujuzi uzoefu na wanapokuwa vyuoni watakuwa wanajifunza kwa vitendo fani ambazo wanazosomea.

Alisema katika kukabiliana na changoto ya vijana kukosa ajira, CBE imeshaanzisha programu atamizi ya biashara kuwawezesha wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo kuwa na ujuzi wa biashara na kujiajiri wenyewe.

Chuo hicho kimeshaingia mkataba na taasisi nyingi zikiwamo benki ili wanafunzi wake waweze kufanyakazi kwa vitendo wakati wanapoendelea kuwa masomoni chuoni hapo.

# LATRA: Sekta binafsi kuanza kuwekeza usafiri wa reli

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema sekta binafsi itaanza kuwekeza kwenye usafiri wa reli nchini na kwamba uandaaji wa kanuni, miongozo itakayotumika umeshakamilika.

Imesema uwekezaji huo utakuwa katika usafirishaji wa abiria, mizigo, lengo kuu ni kuleta ufanisi katika sekta ya usafirishaji nchini.

Pia, imesema imeshaandaa kanuni zitakazotumiwa na wawekezaji watakaowekeza katika safari za magari ya umeme yapitayo juu kwa kutumia nyaya (cable cars) hapa nchini.

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli LATRA, Hanya Mbawala, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha kujengeana uelewa kati ya maofisa wa taasisi hiyo, waandishi wa habari na wahariri.

Kuhusu uwekezaji wa reli, alisema watu binafsi wataanza kuwekeza kwenye sekta hiyo hususani katika usafirishaji wa mizigo na abiria.

"Kanuni tayari zimeshaandaliwa, tumezipeleka kwa waziri ili azipitishe. Hali hiyo itaongeza ufanisi katika usafirishaji wa mizigo na abiria kupitia reli zetu hapa nchini kwa sababu ni asilimia 1.3 ya mizigo yote kutoka bandarini inasafirishwa na reli," alisema. Kuhusu usafiri wa waya, Mbawala alisema tayari kanuni zimeshatengenezwa na zipo kwa waziri, ndani ya kanuni hizo kuna viwango vinavyoeleza namna ya kuwekeza.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema hadi sasa wameshatoa leseni za usafirishaji kwa magari 284,000, kati ya idadi hiyo mabasi ni 50,221, malori 169,942, magari ya kukodi 718, bajaji 20574, pikipiki 31,937, taxi mtandao 3,523.

Pia, hadi kufikia Septemba 30, mwaka huu, wamewasajili madereva 17,990, kati ya hao 1,617 wamefanya mtihani wa LATRA, magari mengi yamefungwa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS). Alisema LATRA pia wameanza kusimamia utoaji wa mafunzo mafupi kwa makondakta kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara, Johansen Kahatano, akizungumzia kuhusu wasafirishaji kupandisha nauli, alisema wanafuatilia hali hiyo na kuchukua hatua.





Kaimu Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la Muheza, Mohamed Kissasi (wa pili kushoto), akizungumza wakati wa mahafali ya 13 ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Kwemkabara, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM kata ya Kwamkabara, Edward Masawe (kulia), Mkuu wa shule hiyo, Juma Hango (wa pili kulia) na (kushoto) ni Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, John Mdoe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hofu yatanda wanafunzi jinsia moja MoCU kulala chumba kimoja

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HOFU imewakumba wadau wanaotoa huduma za malazi kwa wanafunzi wanaolala nje ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kutokana na zaidi ya wawili kuishi chumba kimoja, imefahamika.

Hayo yalifahamika jana wakati Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitandu, Mohamed Mfaume akizungumza kwenye kikao cha wadau hao na Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi ya MoCU kilichokuwa kikijadili namna ya kuboresha huduma za malazi kwa wanafunzi wa chuo hicho.

"Tunaomba wale wanafunzi wenye hali ngumu kimaisha musaidie wapate vyumba ndani ya chuo ili wasiishi zaidi ya wawili, watatu mpaka wanne chumba kimoja huko mitaani.

"Wengi tunawaona huko wanalala pamoja ili kupunguza gharama za malazi. Tunashukuru chuo na serikali mnapambana kukiboresha chuo na huduma za malazi kwa kushirikiana na wadau wenye hosteli."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kariwa Chini, Thomas Matetu, aliwashauri wamiliki wa nyumba zinazotoa huduma ya malazi kwa wanafunzi wa chuo hicho kuweka sheria kali ili kuwabana wanafunzi waliopanga kwao kuacha kulala chumba kimoja zaidi ya wawili.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Wanafunzi wa MoCU, Dk. Elisifa Nnko, alieleza kufurahishwa kwake namna wadau walivyojadili changamoto hiyo na kutoa ushauri wa jinsi ya kukabiliana nayo.

"Nimefurahi maradufu. Katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, tuna sera, sheria na miongozo na taratibu za kuongoza hawa wanafunzi," alisema.

Kati ya wanafunzi 9,000 chuoni hapo, 1,200 wamepata nafasi za malazi huku zaidi ya 7,000 wakiishi nje ya chuo wakiwa wamepanga hosteli.

"Sisi tuna utaratibu wetu mzuri tu ndani ya chuo. Tuna wanafunzi wengi wanaokaa nje ya chuo na ndani ya chuo. Bado tuna wajibu kuwafuatilia na katika chuo hiki, kila chumba wanakaa wanafunzi wanne," alisema na kusisitiza kuwa:

...Tunachokifanya sisi tuna vipaumbele vyetu ambavyo vimewekwa kwenye sera na miongozo. Kipaumbele cha kwanza ni tunawaangalia wanafunzi wenye mahitaji maalumu, lakini cha pili ni wanafunzi kutoka nje ya nchi, kipaumbele cha tatu ni wanafunzi wa kike wa ngazi ya cheti ambao ni wadogo."

Hata hivyo, alisema wameuopokea ushauri wa kupapa nafasi ya kuishi chuoni hapo wanafunzi wenye hali ngumu kimaisha.

## Shule ya Tanganyika yalimwa faini kwa fedha za bima

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imeitoza faini ya Shilingi 5,000,000 shule za msingi na sekondari za Tanganyika mkoani hapa kwa kosa la kukusanya ada za bima za matibabu kwa wanafunzi wao kinyume cha sheria.

Shule hizo zinatuhumiwa kukusanya ada hizo, kati ya mwaka 2014 hadi 2023 kinyume cha sheria za bima.

Aidha, imeiagiza shule hiyo kurudisha fedha iliyokusanya kutoka kwa Alexander Oyuge, kwa muda wote ambao watoto wake walikuwa wakisoma shuleni hapo, kwa kuwa ada hizo hazijatumika kutoa kinga aliyostahili.

Vilevile, TIRA imeiagiza shule hiyo kufanya utaratibu rasmi ili wasajiliwe na mamlaka hiyo, na kuruhusiwa kukusanya ada za bima kisheria, ikiwa ina nia ya kujihusisha na biashara ya bima.

Kukusanya bima bila kibali halali, kinyume na Sheria ya Bima, Sura ya 394 kifungu cha 161 (1).

Akizungumzia sakata hilo, Kamishna wa Bima, Dk.Baghayo Saqware, aliwaomba wananchi kujiepusha kulipa huduma ambayo inatolewa na mtu au taasisi ambayo haijasajiliwa kufanya biashara ya bima.

Alisema shule hiyo hiyo hutoza ada ya bima Sh. 200,000 kwa mwaka kwa kila mwanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari, huku wanafunzi wa Shule ya Awali Sh.90, 000.

Kamishna Saqware, alisema walibaini kwenye uchunguzi wao kuwa shule hiyo imekusanya ada za bima kutoka kwa wanafunzi wa shule ya awali na msingi zaidi ya Sh.milioni 207.600.

"Fedha hizi wamezitumia kununua seti ya huduma kwanza na kuwahudumia wanafunzi kimatibabu wanaopatwa na majanga ya kuumwa wanapokuwa shuleni kuanzia asubuhi hadi jioni wanapomaliza," alisisitiza

# Naibu Waziri awapasha watendaji SIDO, TMDA

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amewaagiza watendaji wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Nchini (SIDO) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwenda kusikiliza kilio cha wafanyabiashara kucheleweshwa uthibitisho wa kisheria wa bidhaa zao.

Kigahe, alitoa maagizo hayo jana katika Mji wa Babati wakati akizindua Maonyesho ya Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Manyara.

"SIDO na TMDA tusisubiri watu watufuate ofisini ili kuthibitisha bidhaa zao, acheni urasimu. Wafuateni na kuwasaidia, maana hawa ndio mabosi wetu," alisisitiza Naibu Waziri huyo.

Alisema zaidi ya asilimia 24 ya pato la taifa linachangiwa na sekta ya kilimo, huku viwanda vikichangia asilimia saba ya pato hilo.


Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, kilimo ndicho chenye fursa nyingi na ndiyo maana serikali imeweka bima ya mazao ili iwasaidie wakulima kurudi shambani wanapopata majanga.

Awali, Mwenyekiti wa TCCIA, Mkoa wa Manyara, Musa Msuya, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutangaza fursa za utalii, madini, viwanda na biashara.

Aidha, Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa Kiwanda cha Mbolea cha Itracom Fertilizers Limited, Dk. Kenneth Masuki, akizungumza mbele ya Naibu Waziri huyo, alisema wao wana fursa kubwa ya uzalishaji wa samadi ghafi tani 150,000, ambayo ikichakatwa inatumika katika mchanganyiko wa kuzalisha mbolea.

Kwa mujibu wa Dk. Masuki, kiwanda hicho kikimaliza ujenzi kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka, sawa na tani 200,000 kwa kutumia mtambo mmoja, kati ya mitambo mitano iliyonayo.

Alisema mikoa ya Manyara, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Singida na Dodoma, itanufaika kwa kiwango kikubwa, iwapo watazalisha mbolea ya samadi.





## Lori laua, dereva atokomea

**Na Said Sindo,** GEITA

MTU mmoja amefariki dunia na mwingine kujeruhiwa baada ya pikipiki waliyokuwa wakisafiria kugongana na lori.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya alasiri katika eneo la Miti ni Dawa la Halmashauri ya Mji wa Geita wakati dereva wa lori hilo lililokuwa likitokea Shilabe akijaribu kukata kona.

Baadhi ya mashuhuda walidai kuwa chanzo cha ajali hiyo ni uzembe na mwendokasi wa madereva wa vyombo hivyo vya usafiri.

Mashuhuda hao waliendelea kudai kuwa baada ya ajali hiyo kutokea, dereva wa lori alitokomea kusikojulikana.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Geita, Dk. Thomas Mafulu alithibitisha kupokea majeruhi hao na kwamba mmoja alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

Alisema mwili wa marehemu huyo umehifadhiwa katika chumba cha maiti kusubiri ndugu kuuchukua kwa ajili ya maziko.

Kadhalika, alisema majeruhi wa ajali hiyo naye bado hajatambuliwa na kuwaomba wananchi ambao hawajawaona ndugu zao kufika hospitalini hapo kuwatambua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo hakuwa tayari kuzungumzia ajali hiyo kwa kile alichoeleza kuwa yuko mkoani Mwanza kikazi.

# Ucheleweshaji mizigo bandarini pasua kichwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Kanda ya Ziwa Victoria imekutana na wadau binafsi na sekta za serikali kujadili kuboresha utendaji kazi na kudhibiti ucheleweshwaji wa mizigo bandarini.

Akifungua kikao hicho jana Meneja wa TPA Kanda ya Ziwa, Wakili Erasto Lugenge alisema kuwa lengo ni kuondoa mizunguko katika usafirishaji mizigo na msongamano.

Katika kikao hicho kilichowashirikisha watumiaji na wasimamizi wa bandari za Kanda ya Ziwa Victoria alisema kuna baadhi ya taasisi katika mamlaka hiyo ambazo zinatekeleza majukumu yake kisheria, lakini zinasababisha ucheleweshwaji wa mizigo na kuwaingizia hasara wafanyabiashara na wasafirishaji.

Alisema mazungumzo na wadau hao yatasaidia kupata suluhu juu ya utekelezaji wa majukumu kisheria bila kuathiri shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara.

"Mfano mtu anasafirisha bidhaa zake kwa ajili ya kuuza Sikukuu ya Krismasi anafikisha mzigo wake mapema bandarini ili upelekwe eneo husika lakini cha kushangaza mzigo unazunguka hapo bandarini unakuja kutoka Desemba 26 unategemea anaenda kuufanyia kazi gani tena? " Alihoji Wakili Lugenge

Alisema kama watoa huduma katika bandari hiyo, wanatakiwa kuwa na ushirikiano na kufanya kazi kama timu mmoja kwa kuweka mazingira mazuri ili wateja waweze kuchukua muda mfupi kupata huduma.

"Kutokujipanga na kushirikiana sisi wenyewe na kuondoa urasimu na ucheleweshwaji wa hapa na pale tutamfanya mteja akose imani na huduma zetu, haijalishi tunafuata taratibu za Bandari,TBS, Uvuvi, Ulinzi, Misitu na nyinginezo, " alisema.

Baadhi ya wawakilishi wa taasisi zinazoshirikiana na bandari katika kutekeleza majukumu yake ziliahidi kutekeleza majukumu ipasavyo ili kutoa huduma stahiki kwa wateja wao.

"Sisi kama wasimamizi wa hali ya hewa katika bandari hizi jukumu letu ni kuhakikisha tunapokea na kutoa taarifa za machafuko au usalama wa hali ya hewa katika anga na Ziwa Victoria lengo likiwa ni kuhakikisha safari zinakuwa salama," alisema Benedict Ogale Msimamizi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Bandari ya Mwanza Kusini.




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kagahe (kulia), akizungumza katika banda la kampuni inayozalisha vinywaji vikali ya Mati Super Brands Ltd, alipotembelea maonyesho ya Tanzanite Manyara Trade Fair mjini Babati, mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mgogoro wawakera wanufaika TASAF, wajenga barabara

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WANUFAIKA 114 wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wakazi wa Mtaa wa Tanesco Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wamejenga barabara na kumaliza mgogoro katika eneo lao na la Usalama wa Taifa.

Wanufaika hao wamejenga barabara hiyo yenye urefu wa kilometa mbili kila siku kwa kulipwa Shilingi 3,000 kwa siku 60.

Barabara hiyo inayounganisha mtandao wa mawasiliano katika mitaa ya Tanesco, Chamaguha Sanjo imegharimu kiasi cha Sh. milioni 27 zilizotumika kulipa ujira wa wanufaika hao na kununua vifaa vya kazi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wanufaika hao walisema kuwa fedha walizopata kwa kujenga barabara hiyo zinawasaidia kujikimu maisha yao mbali na ruzuku wanazopokea kila baada ya miezi miwili.

Mkazi wa Mtaa wa Sanjo, Mushi Ngoyeji, alisema barabara hiyo imewasaidia kutatua migogoro baina yao na serikali kutokana na wananchi kuvamia eneo la Usalama wa Taifa na kuanzisha ujenzi wa makazi ya kudumu na kilimo.

Hata hivyo, alisema awali eneo hilo lilikuwa hatarishi likitumiwa na vibaka kwa kuendesha vitendo vya ukabaji na uporaji mali za wananchi, hivyo ujenzi wa barabara hiyo umesaidia kudhibiti vitendo hivyo.

Aliwapongeza wanufaika wa TASAF kwa kujenga barabara hiyo kwani inawarahisishia kusafirisha mazao yao kutoka shambani hadi sokoni.

Mmoja wa wanufaika hao, Mwita Seleman (71), alisema walihamasika kujenga barabara hiyo ili kudhibiti eneo la serikali kuvamiwa na wananchi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tanesco, Seleman Mzee (63), alisema eneo hilo lilikuwa na barabara, lakini iligeuka kichaka kwa sababu haikuchongwa kwa muda mrefu na kuwa maficho ya wahalifu




Ukurasa 13

Mgeni njoo mwenyeji apone iwe kweli

BUFE

IJUMAA OKTOBA 20, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**UBIA wa NSSF & MAGEREZA**
**Kiwanda kipya kitakachozalisha aina sukari inayoagizwa nje kwa matumizi ya viwandani**

Ukurasa 12

## MAELEKEZO YA RAIS 2025 LENGO LITIMIE...

# Wakala wa Mbegu yaingia kazini kufufua mashamba serikali, nchi ijitosheleze 75%

• Nyenzo: Utafiti, ubia na sekta binafsi, uwekezaji...

**Na Renatha Msungu**



Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mbegu Tanzania, Dk. Sophia Kashenge, akikagua mbegu kutoka kwa mmoja ya wazalishaji wake binafsi. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, anasema serikali inaboresha vituo vya utafiti na mashamba ya uzalishaji mbegu, kutokana na kujiingiza uzalishaji mbegu za kisasa, lengo ni nchi kujitegemea kwa mahitaji ya mbegu.

Akizungumza katika Mkutano Maalumu na Vijana, ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika unaofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 7 mwaka huu, rais akasema serikali imewekeza kwenye utafiti na matumizi ya Mifumo ya Mawasiliano (ICT), ili kukuza uzalishaji mbegu na nafaka.

"Tunataka ifikapo 2025 robo tatu ya mbegu zote zinazotumika hapa nchini zizalishwe hapa kama sio kujitegemea kabisa. Tunataka mbegu zilizothibitishwa na zinazoendana na aina ya udongo wetu pamoja na kustahilimi mabadiliko ya hali ya hewa," anasema Rais, Samia.

Katika soko, rais akasema serikali imefanya ufuatiliaji na tathmini katika mnyororo wa kuzalisha mpaka kuuza mazao mbalimbali na hatua zimeshaanza kutoa matokeo chanya.

"Tunawaunganisha wakulima na masoko kwa kutumia vyama vya ushirika bado hatujafanya vizuri, lakini kwa mazao tuliyoanza nayo kama korosho na mbaazi yanafanya vizuri.

'Mwaka jana, bei ya mbaazi ilikuwa shilingi 300 kwa kilo moja, mwaka huu ikapanda mpaka shilingi 2,000 kwa kilo moja, tunataka twende na utaratibu wa vyama vya ushirika kwa mazao yote ili wanunuzi washindane," anasema.

Vilevile akasema, serikali inafuatilia kujua mahitaji ya mazao kabla ya kuzalisha na kuiswezesha kujua aina ya zao na masoko, huku kukiimarishwa miundombinu ya usafirishaji mazao kwa sekta zote.

Hapo anaorodhesha usafiri wa anga, nchi kavu na majini kama kujenga barabara, ujenzi wa reli ya kisasa, pia kununua ndege ya mizigo na ujenzi wa hifadhi ya mazao yanayoharibika haraka bandarini yakisubiri kusafirishwa,

Anaeleza pia hoja ya kutumia teknolojia ya mawasiliano kwa wakulima wanaosajiliwa na kupatiwa huduma kwenye mifumo ya kuwahudumia, aidha, maofisa ugani wamewezeshwa kwa vifaa maalumu, kama kuchukua taarifa hususan za afya ya udongo na umwagiliaji.

Rais wa Tanzania, anasema serikali imeviboresha vituo vya utafiti na mashamba ya uzalishaji mbegu, kutokana na kujiingiza kwenye masuala ya uzalishaji mbegu za kisasa, lengo ni nchi kuweza kujitegemea kwenye mahitaji ya mbegu.

"Tunataka ifikapo 2025 robo tatu ya mbegu zote zinazotumika hapa nchini zizalishwe hapa kama sio kujitegemea kabisa. Tunataka mbegu zilizothibitishwa na zinazoendana na aina ya udongo wetu pamoja na kustahilimi mabadiliko ya hali ya hewa," anatamka Rais, Dk. Samia.

**ASA NA MAPINDUZI KILIMO**

Dira yake Rais Dk. Samia ni kwamba, iingiapo mwaka 2025, taifa lifikie asilimia 75 ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo nchini,ili kukidhi mahitaji ya wakulima, lengo alilotangaza kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Mifumo ya Chakula, jijini Dar es Salaa, mwezi uliopita.

Hapo Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA), imeshaanza mikakati ya uwekezaji katika kuzalisha mbegu kwa kuongeza na kufufua mashamba ya serikali.

Inatajwa kuwa serikali kuongeza bajeti yake katika kilimo, katika miaka miwili ya fedha ya utawala wake Dk. Samia, imeibua mapinduzi ya uzalishaji katika kilimo, ikichukua sura ya kushindana kimataifa, zao lake sasa ASA imeshaanza uwekezaji kwenye kuzalisha mbegu kwa kufufua mashamba ya serikali, ili kuhakikisha wanashirikiana na wawekezaji wazawa katika uzalishaji mbegu.

Hadi sasa ASA inataja kumiliki mashamba 17 ya serikali ambayo imeshafufua yote, ikiingizwa kwenye mikakati ya kuwezesha uwekezaji na uzalishaji mbegu,

kwa kushirikiana na wadau binafsi, ili

Inaendelea Uk 12

BIASHARA

UBIA WA NSSF & MAGEREZA

# Kiwanda kipya kitakachozalisha aina sukari inayoagizwa nje kwa matumizi ya viwandani

- Tani 50,000 sokoni; ajira 13,000; fedha kigeni 20% kuokolewa
- Pia, kuzalisha umeme megawati 15, nusu yake kuuziwa Tanesco
- Neema jirani; walima miwa 243, kicheko walima vitunguu, nyanya

**Na Elizabeth Zaya**

KWA miaka kadhaa, kumekuwapo mijadala inayohusu upungufu wa serikalini, nchi ina hatua zinazoendelea kuchukuliwa kukiwapo kiasi kikubwa cha sukari kinaingizwa kutoka nje, ikiwamo katika baadhi ya nchi za Asia.

Hapo ndipo ikailazimu serikali kutafuta mbinu za kukabiliana na shida hiyo ili kuwasaidia wananchi wake. Mojawapo ni kuhamasisha uwekezaji nchini na mara moja kukasadikika, kuanzishwa viwanda vya kuzalisha sukari, ikiwamo cha Bagamoyo.

Kabla, wastani wa miaka saba iliyopita kukaripotiwa mkakati wa kuanzishwa kiwanda cha kuzalisha sukari nchini wilayani Kilosa, mwekezaji akiwa Shirika la Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), baadaye kukawapo ukimya mkubwa.

Ni kati ya harakati zinazotawala nchini, huku takwimu za Bodi ya Sukari Tanzania (STB), kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikitaja mahitaji ya sukari nchini ni tani 721,000. Hapo inatambulishwa sukari ya matumizi ya nyumbani ni tani 481,000 wakati ile ya matumizi viwandani ni tani 240,000.

Katika kukidhi haja hiyo, takwimu zinaonyesha kuwa uzalishaji sukari nchini katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulikuwa tani 458,799 za sukari ya matumizi ya nyumbani na kwa upande wa sukari ya viwandani, bado haijaanza kuzalishwa nchini.

Katika kuunga mkono mipango na jitihada za serikali kuongeza kiwango cha uzalishaji sukari ipatikane kwa uhakika, hatua tajwa ya kuanzishwa viwanda vipya zinaendelea kuchukuliwa.

Hapo ndipo kinapojitokeza kiwanda cha sukari, ambacho harakati za kukiasisi zilianza nyuma, kisha kukatawaliwa na ukimya kwa miaka mingi kiasi.

**ILIKOANZA MKULAZI**

Ubunifu wa viwanda vipya, ndio kunashuhudiwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi, kikiwa ni miongoni mwa viwanda vipya ambavyo vimeanzishwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa hiyo ya sukari.

Kiwanda hicho kipya cha sukari cha Mkulazi kilichopo mkoani Morogoro, kinatarajia kuanza uzalishaji wa sukari ya viwandani katika mwaka wa fedha 2023/2024, ikiwa ni miongoni mwa hatua za kuunga mkono juhudi za serikali kupunguza uhaba wa sukari nchini.



Sehemu ya Kiwanda cha Sukari Mkulazi, wilayani Kilosa, Morogoro, kinachotarajiwa kuanza uzalishaji tani 50,000 katika mwaka wa fedha uliopo, pia kuzalisha umeme. Kulia, ni shamba lake la miwa, lenye bwawa la maji. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA.**

Hapo mahsusi inatajwa ni zao la serikali, kuweka mikakati na mazingira wezeshi kwa wawekezaji, kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vipya vya sukari

NSSF ikiwa kwenye ubia na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza (SHIMA), walikubaliana kuanzisha ujenzi wa kiwanda kipya cha sukari cha Mkulazi, mwaka 2016, hisa zikiwa asilimia 96 za NSSF na Magereza, asilimia sita.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo hodhi ya Mkulazi, Selestine Some, anasema inatekeleza mradi wa kiwanda hicho cha sukari katika shamba la Mbigiri, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, kiwanda kikitarajia kuzalisha tani 50,000 cha bidhaa hiyo kila mwaka.

Some anasema, pamoja na kuendeleza Shamba la Miwa la Mbigiri, kuna jumla ya wakulima wa miwa 243 jirani na mradi, ambao tayari wamesajiliwa na Bodi ya Sukari Tanzania na wameshalima zaidi ya hekta 800 za miwa.

Pia, anasema kampuni imewekeza katika ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, ikiwamo mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji kipindi cha mvua na kuyatumia wakati wa kiangazi.

Mtendaji huyo mkuu anaeleza kiwanda cha Mkulazi, ujenzi wake ulianza rasmi, Julai mwaka 2021, akiwa na ufafanuzi kitakapokamilika, kitaweza kuzalisha tani 50,000 za sukari ya viwandani na majumbani kwa mwaka.

**FAIDA ZINAZOTARAJIWA**

"Kiwanda pia kitazalisha umeme kiasi cha megawati 15. Kati ya hizo, megawati nane zitatumika kwenye kiwanda, mashambani na ofisini na nyingine saba zinatarajiwa kuuzwa kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa," anasema Some.

Some anasema kiwanda kinatarajiwa kwamba kitasaidia kupunguza uagizaji sukari ya viwandani kwa asilimia 20, ambayo ni faida itakayookoa matumizi ya fedha za kigeni kwenye

Inaendelea Uk 14

## Wakala Mbegu yaingia kazini kufufua mashamba serikali, nchi ijitosheleze 75%

Inatoka Uk 11

kuhakikisha lengo linafikiwa na fursa zimeshafunguliwa milango katika mashamba ya serikali wanayoyamiliki.

BOSI MKUU ASA

Dk. Shohia Kashenge, Mkurugenzi Mtendaji wa ASA. anasema mikakati yao sasa ni kuhakikisha wanatimiza lengo la serikali kutimu mwaka 2025, kujitosheleza kwa mbegu kitaifa, robo tatu ya mahitaji.

Anataja mikakati hiyo, inajumuisha kushirikiana na wawekezaji wazawa kuzalisha mbegu bora za mazao, zitakazotumiwa na wakulima kwa msimu wa kilimo.

Dk Kashenge anasema, wamezikaribisha sekta binafsi katika uzalishaji mbegu wa mazao, ili kuhakikisha kunauwapo mbegu bora nyingi nchini, zitakaokidhi mahitaji ya wakulima na kuzisambaza kwa wakala wake.

Anasema, tayari ASA imeshaanza mchakato wa kutayarisha mashamba kwa ajili ya wadau na kuyatumia kwenye uzalishaji, akifafanua:

"Hivi sasa fursa ziko 'nje nje' katika uzalishaji mbegu., Tunawaomba sekta binafsi na wawekezaji wazawa wajitokeze kwa ajili ya kuchangamkia fursa za uzalishaji mbegu," anasema Dk. Kashenge.

"Naomba wawekezaji wazawa mjitokeze katika kuwekeza kwenye uzalishaji mbegu, tunahitaji kuona tunafikia malengo serikali iliojiwekea katika suala zima la uzalishaji mbegu," anatamka.

**VIJANA NA MBEGU**

Ushauri wake Dk. Kashenge, ni kwa vijana wengi wajitoe kujikita kwenye kilimo cha uzalishaji mbegu, kwa sababu kuna uhitaji wa bidhaa bora nyingi za mazao, kutokana na kutanuka umuhimu wa kilimo sasa.

Anatumia mfano wa vijana waliohitimu mafunzo ya 'Jenga Kesho iliyo Bora' au BBT, nao wanapewa nafasi kubwa, kutokana na kufundishwa kilimo, katika mkakati walionolewa na serikali, huko Bahi Dodoma, kwenye mashamba maalum.

"Vijana wa BBT nao tunawakaribisha, kwa sababu kilimo wanakijua, wanaweza kujikita pia katika uzalishaji wa mbegu, kwa sababu wakiwa kwenye mafunzo, ASA ilikwenda kuwafundisha namna ya uzalishaji mbegu bora," anasema Dk Kashenge.

Sasa anawageukia kwea ushauri kwamba, ni wakato kwa vijana hao wakatumia fursa hiyo kuhakikisha wanashirikiana na ASA kuzalisha mbegu bora za mazao ya kilimo nchini.

"Uzalishaji mbegu nao ni kilimo. Hivyo vijana wa BBT nao wanawezakujitokeza kusaidia katika uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo," anasema Dk Kashenge.

Anafafanua kuwa,wawekezaji watakaojitokeza, wao ASA wakiwa Wakala wa Mbegu za Kilimo, watakaa nao chini kukubaliana namna ya kuzalishaa mbegu, ikiwamo kuwapa maelekezo yanayohakikisha wanazalisha mbegu bora kutumiwa nchini.

**WAZIRI KILIMO BASHE**

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anataja mikakati yao ya kiserikali ni kuhakikisha kilimo kinakuwa kwa kiasi kikubwa nchini, kutimiza ajenda na kuchangia asilimia kubwa katika pato la taifa.

Bashe anasema, taasisi za kilimo zinatakiwa kusimama imara kuhakikisha wanazalisha mbegu bora za kilimo kwenye mazao mbalimbali, kuhakikisha wakulima wanazipata kwa wakati.

Anasema lengo lao, ni kuona kilimo chenye tija shambani, kinachowainua wakulima kiuchumi na familia zao.

**WANENAVYO WAKULIMA**

Inajulikana, changamoto kubwa katika kilimo shambani ni kwenye mbegu bora, wanaipongeza ASA kutoa fursa za kushirikiana na sekta binafsi kuzalisha mbegu.

Mkulima Mamvula Khamis, kutoka kijiji cha Mvumi mkoani Dodoma, anaisifu ASA imefanya vizuri kuita wawekezaji wazawa watakaoshirikiana na mashamba ya serikali kwenye uzalishaji mbegu za mazao.

Anaahidi kitakuwapo changamoto ya upatikanaji mbegu kwa wakati, kutokana na kuzalishwa kwa wingi na wakala hao, kwa kushirikiana na sekta binafsi zinazozitangazia fursa katika uzalishaji mbegu.

Mkulima John Matonya, anaeleza suala la uzalishaji mbegu bora za kilimo kwa wingi, zina sifa ya kuwanufaisha kwa kiasi kikubwa, kwa sababu wakulima watazipata kwa wakati kabla ya msimu wa kilimo kuwadia.

"Nawapongeza sana ASA kwa hii mikakati waliyoianzisha, waendelee nayo ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiweka katika uzalishaji wa mbegu bora zitakazotumika kwenye msimu wa kilimo," anasema Matonya.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mgeni njoo mwenyeji apone iwe kweli






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

USEMI wa mgeni njoo mwenyeji apone ni maarufu sana katika jamii na familia za kiswahili, hususan kwa walio masikini wanaoamini katika ujio wa wageni, unaokoa maisha yao.

Unanikumbusha jinsi baadhi ya familia zinavyochangamka au kubadilika mara zipatapo ugeni, kwani maisha hubadilika ghafla na kuwa ya bandia mpaka mgeni aondokapo.

Mathalan, usafi hufanywa hata mahali ambako haukuwa ukifanyika, chakula hubadilika, mavazi hubadilika, lakini hata vyombo vya chakula vinabadilika.

Ndiyo siku kabati za nguo na vyombo hufunguliwa, ili angalau wenyeji kujifaragua na kuonekana hawana matatizo na hivyo wasionekane wanyonge kwa wageni.

Kwa Watoto, ndio hasa wanashukuru ujio wa ugeni, kwani wanafaidi chakula tofauti, kwani mgeni anapochinjiwa mathalan kuku, hata watoto siku hiyo hubadili chakula na kuambulia miguu, shingo au vipapatio vya kuku.

Ni siku ambayo pengine nguo walizonunuliwa mwaka jana kwa sikukuu, hutolewa kabatini na kuvaa, ili kuonekana watanashati kwa wageni. Hiyo ni hali inayotawala zaidi familia zetu za 'pangu pakavu tia mchuzi'.

Safari hii mgeni njoo mwenyeji apone imetukuta Watanzania, baada ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kutukubalia kuandaa michuano ya Ligi ya Mpira wa Miguu Afrika (AFL).

Uwanja wetu wa Benjamin Mlkapa, utakuwa na mshikemshike wa michuano hiyo, huku leo ukishuhudia kuzinduliwa kwa michuano hiyo kati ya Simba na Al Ahly ya Misri.

Ujio wa michuano hiyo, umesababisha uwanja huo kufanyiwa ukarabati wa nguvu, licha ya mwingine kuwahi kufanyika awali, lakini kichovu. Safari hii Kwa Mkapa kunaonekana kwa kimataifa zaidi kutokana na ukarabati unaofanyika.

Pengine bila michuano hiyo, uwanja huo ambao ni mkubwa kuliko vyote nchini, ungejiharibikia, hivyo hivyo na hatimaye kubaki gofu, kwani Wabongo tunajuana katika kutunza miundombinu yetu.

Ni sisi ambao kila ujenzi wa miundombinu ukamilikapo na kuzinduliwa kwa matumizi, lazima viongozi watuhadharishe, kutukumbusha na kutusisitiza kuitumia vizuri na kuitunza, kwa sababu tunajulikana ni kama sisi ni hamnazo.

Ni katika uwanja huo huo ambako Wabongo waliingia maliwatoni na kung'oa koki za mabomba, wakati uwanja hata haujatimiza umri wa miaka mitatu na hata wengine kujisaidia kwenye masinki ya kunawia.

Katika uwanja huo pia, kuna mashabiki wa timu moja kubwa ambao baada ya kufungwa, wakachukia viti na kuving'olea mbali kwa hasira, kana kwamba ndivyo vilikuwa vikifunga mabao au vikiyaruhusu kuingia langoni mwa timu yao.

Sasa uwanja huu unaheshimika kutokana na ukarabati uliofanywa na unaoendelea kufanywa, tukitarajia kuwa utatunzwa nasi na hata ikija michuano mingine ya kimataifa basi utumike.

Kutokana na ubora wake, tulishashuhudia timu nyingi za kimataifa zikiomba kuutumia kama uwanja mwenyeji na sasa tunasikia TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) imeomba kuutumia. Tunasikia pia kuna miamba ya Sudan nayo imeomba hivyo hivyo kuutumia, hii ikionyesha ukubwa na ubora wa uwanja, pia imani kimataifa tuliyo nayo Wabongo, ingawa kama hatujajitambua bado.

Ni imani yangu, kuwa changamoto zilizokuwapo awali zikiwa ni pamoja na watu kutojali namba za viti na kujikalia wanavyojua, kusimama kwenye viti kushangilia magoli na baadhi ya malango kutofunguliwa, zitakoma.

Kwamba huko maliwatoni sasa, tutakuta watu wameweka viti vyao kwa ajili ya kusafisha kila yanapotumika, badala ya kusubiri maelfu ya watu wametumia na kuja kusafisha kesho yake.

Sijaingia viwanja vingi vya michezo duniani, lakini nathubutu kujishaua kuwa nimeingia viwanja vingi vya ndege duniani, ambako unakuta mtu maliwatoni akisafisha muda wote wanapoingia abiria na kutoka kujisaidia.

Kwani hapo Kwa Mkapa, hatuwezi kufanya hayo? Kwamba menejimenti ya Uwanja wa Mkapa, iajiri watu mahususi kwa ajili ya maliwato tu. Wa kulinda miundombinu hiyo dhidi ya wavuta bangi wetu, lakini pia kuisafisha.

Tuondokane pia na watu wanaosimama malangoni kuchukua chochote kitu na kuingiza watu waliolipia mzunguko na badala yake wakakae kwa watu maalumu au muhimu (VIPs).

Tumheshimu mgeni huyo aliyekuja, ili tupone na hizi nguo mpya tunazovaa, hiki chakula kizuri tunachokula, vyombo vya chakula tunavyotumia na haya mazingira tunayosafisha, viwe vya kudumu, si akiondoka tu tuvirudishe kabatini na kuendelea kula ugali na msunga. Kila la heri Mnyama leo!

UCHUMI

# TASAC yatangazia vijana neema ya ajira katika sekta ya usafiri

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) likijivunia mafanikio ya kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 43 na kuchangia pato la taifa katika kipindi cha miaka mitano, limetangaza kufungua milango kwa vijana nchini ya kwenda kupata ushauri wa namna ya kupata mitaji na kuchangamkia fursa ya kujiajiri katika sekta ya usafiri wa maji nchini.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa TASAC, Nelson Mlali wao kama shirika wapo kwa ajili ya kuwaonyesha njia vijana ya kupata mitaji kukuza uchumi wao kwa kujiajiri katika fursa walizotangaza

" Kama taasisi ya Serikali tutakuwa tayari kutoa ushauri kwa vijana watakaokuja ofisini kwetu kuomba ushauri wa jinsi ya kupata mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za fedha nchini ili waweze kujiajiri," anasema Mlali na kuongeza kuwa:. "Jukumu la kutoa mitaji ni la taasisi za fedha."

Anazitaja fursa hizo kuwa ni kuanzisha usajili wa meli kwa masharti rafiki, maeneo ya ukarabati na ujenzi wa meli katika Ukanda wa Pwani.

Mlali anaendelea kutaja fursa nyingine kuwa ni uanzishwaji wa maegesho ya boti ndogo, viwanda vya utengenezaji malighafi za ujenzi wa boti za plastiki, bandari rasmi za uvuvi na kukidhi mahitaji ya soko la Comoro.

"Sensa ilibaini idadi ya vyombo vidogo vya majini ni 52,189 kati ya vyombo hivyo, vidogo vya majini ni vyenye urefu wa mita nne na zaidi ni 45,976 sawa na asilimia 88," anasema.

Hata hivyo, anasema pamoja na kuwepo kwa fursa hizo, TASAC inaendelea kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya haraka ya teknolojia katika sekta yanayoendelea kutokea duniani na mahitaji makubwa ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Anasema pia kuna uhaba wa



Meli zinazohudumiwa na TASAC, zikiwa bandarini. **PICHA:MAKTABA.**

wataalamu wa ndani katika baadhi ya taaluma hasa wakaguzi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini.

Anasema kwa kushirikiana na vyuo na taasisi vinavyotoa mafunzo ya ubaharia kikiwemo Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), TASAC inatarajia kuongeza uwezo na wigo wa kutoa mafunzo na kuzalisha wataalamu wanaohitajika.

Pamoja na DMI, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), pia kinatoa mafunzo kwa wataalamu hao.

Akizungumza kuhusu mafanikio ya TASAC kukusanya kiasi hicho cha Shilingi bilioni 43, Mlali anasema kilipatikana kuanzia mwaka wa fedha wa 2019/2020 hadi mwaka 2021/2022.

Anasema kiasi hicho ambacho ni ongezeko la mchango mkuu wa serikali kilikusanywa katika kipindi hicho kutoka zaidi ya Shilingi bilioni 9.1 hadi Shilingi. bilioni 43. 4.

Mlali anafafanua kuwa shirika hilo ambalo lilianzishwa Februari 23, mwaka 2018, lilikusanya Shilingi bilioni 9.1 katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Shilingi bilioni 20.1 2019/2020 na Shilingi bilioni 31.8 mwaka 2020/2021.

Anasema kiasi cha Shilingi bilioni 43.4 kilikusanywa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022.

Mlali anayataja mafanikio mengine ambayo TASAC imeyapata kwa kipindi hicho kuwa ni kuongeza idadi ya kadhia zilizohudumiwa kutoka 6,000 hadi kufikia zaidi ya 10,000.

Vilevile TASAC iliunda nyenzo za udhibiti wa usafiri majini ikiwa ni pamoja na Kanuni na Miongozo ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria katika kudhibiti usafiri majini.

Imeongeza idadi ya watoa huduma wanaodhibitiwa na TASAC kwa maana ya idadi ya leseni na vyeti vya usajili vilivyotolewa, idadi ya vyeti kwa mabaharia waliokidhi masharti kutoka 5,699 hadi 17,689.

Anasema pia shirika hilo liliongeza kutoa dadi idadi ya leseni za vyombo vidogo vinavyotoa huduma za usafiri majini kutoka 2,000 hadi 6,366, ukaguzi wa meli za kigeni na mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Vilevile, shirika hilo liliimarisha udhibiti wa huduma za bandari baada ya urasimishaji wa maeneo 20 katika mwambao wa Bahari ya Hindi na maziwa nchini.

Anasema shirika hilo pia liliendelea kusimamia utekelezaji wa mikataba, itifaki na miongozo inayotolewa na Shirika la Bahari Duniani (IMO) na kuridhiwa na serikali.

Pia lilifanikiwa kuzuia na kupambana na umwagikaji wa mafuta baharini, kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2018/2019 hadi 2020/2021.

" TASA imekuwa miongoni mwa taasisi 10 bora nchini katika mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)," anasema.

Anasema mafanikio hayo yamepatikana kutokana na serikali kupokea ushauri wa kitaalamu, miongozo na maelekezo sahihi kupitia Wizara ya Uchukuzi na kamati za Bunge na ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya usafiri kwa njia ya maji nchini.

Akizungumzia matarajio ya TASAC anasema shirika linaendelea na utekelezaji wa mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi Ziwa Victoria unaotarajiwa kukamilika Desemba mwakani.

Mlali anasema wana mpango wa ujenzi wa boti tano za uokozi, mbili zitakuwa Ziwa Victoria, nyingine mbili Ziwa Tanganyika na moja Ziwa Nyasa.

Akizungumzia sababu za kujengwa kwa boti hizo katika maziwa hayo nchini, anasema wameamua kufanya hivyo kwa sababu mazingira ya Bahari ya Hindi na maziwa kuwa tofauti.

Anasema katika maziwa kumekuwa na ajali nyingi zikitokea, kwani wanafanya hivyo ili kuwepo na vyombo vingi vya uokoaji na kunusuru maisha ya watu.

"Kwenye maziwa wenyewe ni mashahidi, mumekuwa mkisikia ajali nyingi zinatokea na kusababisha watu kufa... kwa hapo baharini kuna kituo cha kuratibu matukio Feri na askari wa Navy (kikosi cha wana maji cha Jeshi la Polisi)," anasema na kusisitiza kuwa:

"Tumeona kwanza tuanze na maziwa, baadaye tutaangalia baharini kwa sana kuna vyombo vingi vya uokozi."

Akizungumzia kuhusu Shirika la Suma JKT, anasema anaingia Bandarini kutoa huduma kama mashirika mengine.

Kupitia TASAC, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini Hati ya Makubaliano (MOU) ya kutambuliana vyeti vya mabaharia na nchi ya Barbados Oktoba 3, mwaka huu.

Hadi sasa Tanzania imeanzisha mawasiliano na majadiliano na nchi 34 kwa ajili ya kuingia katika makubaliano ya kutambuliana vyeti vya ili kufungua fursa ya ajira kwa mabaharia wa nchini kuondoa usumbufu wa kushushwa kwa mabaharia wa Kitanzania katika meli ambazo zimesajiliwa na nchi ambazo haina mkataba nazo.

Nchi nyingine ambazo Tanzania imeanzisha mawasiliano na majadiliano nazo ni pamoja na Bahamas, Algeria, Korea ya Kusini, China, Comoros, Cyprus na Misri.

Nyingine ni Ufaransa, Ghana, India, Iran, Kenya, Liberia, Malta, Marshall Islands, Mongolia, Oman, Palau, Panama, Peru, Qatar, Saudi Arabia, Singapore, Africa Kusini, Sycheles, Uturuki, Umoja wa Falme za Kiarabu, Vanuatu, Vietnam na nchi za Umoja wa Ulaya (EU).

Makao makuu ya TASAC yapo jijini Dar es Salaam na ofisi nyingine zipo katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Kigoma, Rukwa, Mtwara, Geita, Kagera, Mara, Lindi, Mbeya-Kyela na Mwanza-Ukerewe.

TASAC pia ina ofisi za mipakani zilizopo mikoa ya Kilimanjaro (Holili), Kagera (Mutukula), Mbeya (Itungi & Kiwira), Rukwa (Kasanga & Kipili), Tunduma, Katavi (Kalema), Mbambabay, Horohoro, Namanga, Kilwa na Sirari (Mara).

## Kiwanda kipya kitakachozalisha aina sukari inayoagizwa nje kwa matumizi ya viwandani

Inatoka Uk 12

kununua sukari ya viwandani.

Mtendaji huyo anaeleza mpaka kufikia Agosti mwaka huu, kiwanda kimeshatoa ajira za moja kwa moja kwa watu zaidi ya 1,300 huku ajira zisizo za moja kwa moja zimetolewa kwa Watanzania wanaokadiriwa, ni zaidi ya 4,600.

Some anaendelea: "Kiwanda hiki kitakapokamilika, kinategemea kutoa ajira za moja kwa moja kwa wafanyakazi zaidi ya 2,315 na ajira ambazo sio za moja kwa moja zinakadiriwa kufikia zaidi ya Watanzania 9,000. Hii ina maana jumla ya ajira zote zitakazotokana na kiwanda hiki zitafikia 11,315".

Some anasema tayari Kampuni Hodhi ya Mkulazi, imeshaanza kulipa kodi na hadi kufika Agosti mwaka huu, ilikuwa imelipa Sh. bilioni 7.3 na kitakapoanza uzalishaji, wanatarajia kiwango cha ulipaji kodi kitaongezeka.

"Kwa hiyo, uanzishwaji wa kiwanda hiki ni muhimu sana kwa nchi yetu, kwa sababu si tu kinazalisha sukari, lakini yapo manufaa mengine mengi ambayo yanapatikana. Kinazalisha sukari, kinatoa ajira na kinalipa kodi," anatamka Some.

"Niendelee kuishukuru na kuipongeza serikali kwa kutenga fedha na kuanza ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 50 kwenye mashamba ya miwa ya wakulima wa nje. Barabara hii itasaidia usafirishaji wa miwa kutoka kwenye mashamba ya wakulima kwenda kiwanda cha sukari.

"Barabara hii itafungua fursa kubwa za kiuchumi kwenye vijiji vya Mbigiri, Msowero, Mabana na Mambegwa. Itatumika pia kusafirisha mazao mengine yanayolimwa katika vijiji hivyo kama vile mpunga, nyanya na vitunguu kwenda katika masoko ya miji ya jirani na tunaona itakuwa mkombozi mkubwa kwa wakulima," anaeleza.

Anataja kuwa, kampuni hiyo ya kuzalisha sukari, Mkulazi, pia imefanikiwa kujenga zahanati ya kisasa inayotoa huduma za matibabu kwa wafanyakazi na wananchi waishio jirani na kiwanda.

"Tunafanya haya yote ikiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali inazofanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wake," anasema Some.



# Wawekezaji wazawa, wageni waitwa kuwekeza Dodoma

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amewaomba wawekezaji kutoka ndani na nje ya Dodoma kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizopo kutokana na kuwapo mazingira mazuri ya kujiinua kiuchumi.

Senyamule alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua semina ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje waliopo Dodoma kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Alisema kuwa fursa za uwekezaji Dodoma bado ni nyingi hivyo, wanatakiwa kuchangamkia kwa kuwekeza kwenye miradi ikiwamo ujenzi wa majengo ya hoteli za kitaifa, shule, hospitali barabara, maduka na maeneo ya burudani.

Alieleza kuwa Mkoa wa Dodoma ni wa kimkakati na wawekezaji lazima watamani, hivyo wanatakiwa kuutamani kwenye kuwekeza kiuchumi na wakimbilie kuwekeza.

"Dodoma ni makao makuu wa chama na serikali, hivi sasa kuna kila aina ya uwekezaji unaoweza mkawekeza kwenye sekta mbalimbali ikiwemo katika kilimo, elimu, afya, barabara ujenzi wa mahoteli, kumbi za burudani na katika uchimbaji wa madini," alisema.

Pia, aliwataka kuweka mazingira mazuri kwenye uwekezaji wao ili kuleta ushindani wa masoko.

Naye, Meneja wa Kanda ya Kati wa TIC, Venance Mashiba alisema kuwa malengo ya semina hiyo ni kujengena uwezo wa kielimu na mbinu za kibiashara ili kuinua kiuchumi mkoa huo.

Alisema kuwa wawekezaji hao wamekutana kwa lengo la kupeana elimu na mbinu za uwekezaji juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa kuhusu mabadiliko na uboreshaji wa kwenye uwekezaji.

Katibu Tawala Msaidizi Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mwajabu Nyamkomora alisema kuwa wawekezaji wa ndani na nje waliopo Dodoma wamejipanga kutekeleza katika kukuza sekta ya uwekezaji wa uchumi wa juu wenye tija.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, John Kayombo (kulia), akimsikiliza mmoja wa wananchi aliyezungumza kwa niaba ya wengine waliojitokeza kwenye kliniki ya ardhi kwa ajili ya kupata huduma zinazohusiana na migogoro ya ardhi, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Migogoro ya ardhi 1,000 yapokelewa ndani ya siku 3

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIKA kutatua migogoro ya ardhi iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kliniki ya ardhi imepokea malalamiko 1,014 kutoka kwa wananchi, huku 240 wakipatiwa hati miliki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Kayombo alisema kati ya idadi hiyo ya wananchi waliowasilisha malalamiko 514 wamesikilizwa.

Alisema kliniki hiyo ilianza Oktoba 16, mwaka huu na itaendelea hadi leo, huku akiwataka wananchi kuwa na subira ili kutatuliwa kero zao za ardhi.

Alibainisha kuwa wanafanya hivyo ili kuhakikisha wanatatua migogoro ya ardhi ili wananchi wamiliki ardhi kihalali.

Alisema lengo la halmashauri ni kuhakikisha wananchi wa Dodoma hawalii kwa sababu ya ardhi na kuongeza kuwa mkakati huo ni maelekezo ya Rais Samia kuwa hataki kuona wananchi wa Dodoma wanatoa machozi kwenye ardhi.

Naye, Mkazi wa Dodoma, Jonisia Luhigwe alisema kliniki hiyo itasaidia kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

Alisema kliniki hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi ya namna ya kuwa hati miliki ili kuepuka usumbufu wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi kwa wananchi.

Aliomba halmashauri kufanya mchakato huo kuwa endelevu ili kuwasaidia wananchi wasikumbane na migogoro yoyote ile kwenye masuala ya umiliki wa ardhi.

# Ofisi ya Waziri Mkuu yapongezwa utoaji fidia kwa wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imepongezwa kwa kuendelea kuimarisha ustawi wa wafanyakazi wanaopata madhila kazini kwa kuwalipa fidia zinazotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye kikao cha kamati hiyo na menejimenti ya WCF cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mfuko huo, mafanikio na mikakati ya kukabiliana na changamoto.

Aidha, alisisitiza elimu kwa kina kuhusu mafao yanayotolewa na mfuko huo yanapaswa kuelezwa kwa wananchi ili watambue namna ya kufuatilia stahiki zao pindi wanapopata madhira kazini.

Naye, Waziri wa Nchi wa Ofisi hiyo, Prof. Joyce Ndalichako, alihakikishia kamati kuwa WCF itaendelea kutoa elimu kwa umma ili kupata huduma zinazostahili wanapopata madhira yeyote wakiwa kazini.

Aidha, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Patrobas Katambi, alisema kwa mujibu wa sheria kila taasisi ambayo inaajiri inapaswa kujisajili WCF na lengo la mfuko ni kusajili wanachama 3,000 kwa mwaka.

Aidha, Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja, aliahidi kamati kuwa ofisi hiyo itaendelea kuisimamia WCF kuzingatia ushauri na maoni ya kamati hiyo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema kwa mwaka 2022/23 madai 4,306 yalichakatwa na kutoa mafao ya Sh.bilioni 17.9 na imechangiwa na kuongezeka kwa uelewa kwa jamii.

Alisema madai 207 yalikataliwa kwa kukosa vigezo vya fidia ikiwamo kuwasilishwa kwenye mfuko nje ya muda unaotakiwa kisheria na madai mengine kutokuwa na uhusiano na majanga yanayotokana na kazi.

# Silaa aagiza kufutwa hati ya kiwanja alichouziwa m/biashara

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amemwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida, Shamim Hoza, kufuta hati ya kiwanja alichouziwa mfanyabiashara, Philipo Masawe ambacho ni mali ya Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA).

Mfanyabiashara huyo aliuziwa kiwanja hicho Sh.milioni 50 kwa kutumia nyaraka za kughushi.

Alitoa agizo hilo juzi na baada ya maamuzi hayo kuyatangaza hadharani kwenye mkutano wa hadhara uliokuwa umeandaliwa kwa ajili ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhutubia wananchi mjini Singida.

Silaa alifikia maamuzi hayo baada kufanya kikao katika ofisi ya Kamishna kusuluhisha mgogoro wa kiwanja hicho namba 2 kitalu A kilichopo eneo la Manga Manispaa ya Singida ambacho pia kilihudhuriwa na mfanyabiashara huyo na kubaini aliyemuuzia aliyefahamika kwa jina moja la Abubakari alitumia nyaraka za kughushi.

Katika kikao hicho, wanawake wawili Binamu Sagaa na Fatuma Issa waliodaiwa kuweka saini kwenye muhtasari wa mauziano walikana mbele ya waziri kwamba hawakuhusika kabisa na kwamba saini zao zimeghushiwa kuhalalisha uuzwaji wa kiwanja hicho.

"Masawe hapa ndugu yangu unetapeliwa namwagiza Kamishna wa Ardhi Mkoa Singida kupitia Kifungu cha 99 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi afute hati aliyopewa na atoe hati mpya kwa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Singida.

Silaa alisema watu wanapaswa kuwa makini wasitapeliwe pindi wanaponunua ardhi kwa sababu sheria zipo wazi kwamba mali zote za taasisi iwe ya dini au chama haiwezi kuuzwa na mtu binafsi.

Naye mfanyabiashara huyo katika kikao hicho alijitetea kuwa hakatai maamuzi ya serikali ya kufutiwa hati ya kiwanja hicho lakini kwa sababu kuna gharama amezitumia kukiendeleza afikiliwe.

Hata hivyo, Waziri Silaa alimwambia mfanyabiashara huyo kwamba gharama zote alizozitumia amdai Abubakari aliyemuuzia kiwanja hicho kwa kutumia nyaraka feki.








Maofisa wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mkoa wa Mbeya, wakibomoa nyumba zilizojengwa kwenye hifadhi ya barabara ambazo asilimia kubwa ya wamiliki walishalipwa fidia katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani humo juzi, ili kuruhusu mkandarasi anayejenga barabara ya njia nne kuendelea na kazi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbaroni tuhuma kuzusha taharuki ugonjwa wa surua

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKAZI wa Kijiji cha Nkasu wilayani Chunya mkoani Mbeya, Nyibe Matondo anashikiliwa na vyombo vya dola kwa tuhuma za kuzusha taarifa za uwepo wa ugonjwa wa surua kijijini hapo.

Matondo alisambaza taarifa hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii akieleza kuwa katika kijiji hicho imeshika kasi kiasi kwamba karibu kila mji una mgonjwa mmoja wa ugonjwa huo.

Kwenye taarifa hiyo aliambatanisha na picha ya mtoto aliyelala kitandani huku akieleza kuwa ugonjwa huo umesambaa kwa kiwango cha asilimia 78, huku akisisitiza kuwa baadhi ya watu wanakufa kutokana na kukosa fedha za matibabu.

"Mama mwambieni hata wagonjwa awakumbuke siyo Simba na Yanga tu, atoe fungu watu wapate matibabu pia na Chanjo, watu wanapoteza maisha kwa kukosa pesa ya kujihudumia," aliandika Matondo.

Akizungumza na wandishi wa habari juzi, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka alisema baada ya taarifa hizo kusambaa kwenye mitandao ya kijamii wataalamu kutoka katika ofisi yake kwa kushirikiana na wataalamu kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa walikwenda katika kijiji hicho kwa ajili ya kujiridhisha.

Alisema walipofika kwenye kijiji hicho hawakukuta mgonjwa hata mmoja mwenye ugonjwa huo na wala hakuna taarifa zozote za kifo chochote kilichotokana na ugonjwa huo.

Mayeka alisema alivielekeza vyombo vya dola vimsake na kumkamata mtu huyo ili aeleze sababu za kuandika na kusambaza taarifa hizo za uzushi ambazo zilizua taharuki miongoni mwa wananchi.

"Sasa hivi anaendelea kushikiliwa, vyombo vyetu vya dola vinatusaidia kumhoji ili tujue nia yake ilikuwa nini, lakini pia tutachukua hatua zingine za kisheria dhidi yake kwa sababu zipo sheria zinazosimamia masuala ya taarifa za mtandaoni," alisema Mayeka.

Aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kutokuwa na hofu kuhusu ugonjwa huo na badala yake waendelee na kazi zao za uzalishaji mali kwa maelezo kuwa wataalamu wamethibitisha kuwa hakuna ugonjwa huo.

Mayeka alisema serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wananchi wanaendelea kuishi kwa amani na utulivu ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana.

# Viongozi watakiwa kudhibiti utoroshaji mbolea mipakani

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Antony Diallo amewataka viongozi kudhibiti utoroshaji wa mbolea ya ruzuku mipakani, ili kuimarisha agenda ya kitaifa ya kuhakikisha kilimo kinaongeza mchango kwenye uchumi wa nchi.

Diallo alisema watendaji wanapaswa kuhakikisha ruzuku inawafikia wakulima kwa wakati na wanapambana na uhalifu hasa katika kuvusha/ kutorosha mbolea nje ya nchi.

Dk. Diallo amewaomba viongozi hao kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha mbolea hizo zinawafikia wakulima mpaka ngazi ya kata na hivyo kuifanya dhana ya ruzuku kuleta maana kwa kupunguza adha ya wakulima kusafiri mwendo mrefu kufuata mbolea.

Aidha, Dk. Diallo alisisitiza suala la usahihi wa tarifa na kueleza kuwa kumekuwa na tofauti ya taarifa kati ya zile zinazotolewa na mawakala wa mbolea na zile zinazopatikana katika ngazi za kata na wilaya na kuwataka watendaji kutumia taaluma zao vizuri katika kuhakikisha usahihi wa takwimu ili watendaji kufikisha pembejeo za kilimo zinazokidhi mahitaji halisi ya wakulima.

Hivyo, aliwaomba viongozi kushiriki katika kuhakikisha mbolea zinawafikia walengwa na kutimiza nia ya serikali ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa Watanzania.

Pamoja na hayo, Dk. Diallo aliwaomba viongozi hao kuhakikisha wanasimamia ipasavyo matumizi ya vifaa vya kupimia afya ya udongo vilivyotolewa na Serikali kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kujua afya ya udongo, hivyo kuwawezesha kutumia mbolea sahihi kulingana na mahitaji ya udongo na mmea.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliwataka viongozi hao kutilia maanani suala zima la usajili wa wakulima na kushauri vyombo vya habari vitumike katika kuwahamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kujisajili na kuhuisha taarifa zao kwa wale waliojisajili msimu uliopita wa kilimo na kubainisha hakuna mbolea itakayouzwa nje ya mfumo wa ruzuku.

Aidha, aliwaomba mamlaka kuhakikisha mbolea inafika kwa wakati, ikiwa inatosheleza mahitaji ya wakulima kabla ya msimu ili kufanya maandalizi ya msimu wa kilimo kwa wakati na hivyo kuongeza tija kwa wakulima.

Pia, alisisitiza na kuwasihi maofisa ugani kusimamia suala la kupima afya ya udongo kutokana na umuhimu wake utakaowawezesha wakulima kujua aina ya mbolea inayopaswa kutumika na kuongeza uzalishaji ndani ya mkoa.

# Wanafunzi 300 wafadhiliwa kusoma kilimo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 300 kutoka familia duni wamefadhiliwa kusoma masomo ya kilimo katika vyuo mbalimbali vya kilimo nchini katika kipindi cha miaka minne, kupitia programu ya kilimo viwanda.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa kutoa ufadhili huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, Obinna Anyalebechi, alisema wanafunzi wengine watano kwa mwaka huu wamepata ufadhili kupitia programu hiyo inayolenga kutoa fursa ya elimu kwa wanafunzi wasio na uwezo.

"Katika miaka minne iliyopita, programu ya kilimo viwanda imesaidia zaidi ya wanafunzi 300 katika harakati zao za kusomea masomo ya kilimo, huku ikijenga mfumo endelevu wa wataalamu wenye ujuzi ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya kilimo nchini," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mwaka huu wamewasaidia wanafunzi wapya watano ambao watajiunga na wanafunzi wengine tisa ambao tayari wanasomea taaluma za kilimo katika Shule ya St. Maria Goretti iliyopo mkoani Iringa.

Aliongeza kuwa upanuzi huo wa programu unaonyesha dhamira ya kampuni kusaidia utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya sekta ya kilimo, huku lengo kuu likiwa kuongeza uzalishaji na mapato ya wakulima.

Mkurugenzi wa mnyororo wa ugavi wa kampuni hiyo, Alfred Balkagira alisema: "Programu hii inachochea vipaji vya ndani, ikiongeza uwezo wa upatikanaji wa malighafi za ndani. Hatua hii siyo tu inapunguza gharama bali pia inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa jamii za wakulima zinazozunguka, ikijenga uhusiano thabiti kati ya SBL na jamii ya eneo hilo".

Alisisitiza kuwa wanafunzi wanaosoma kupitia programu hiyo huenda wakawa mabingwa wa mbinu endelevu za kilimo na hivyo kuathiri kwa njia chanya mchakato wa upatikanaji na uzalishaji.

# Mbunge ashauri kuongezwa idadi lugha za kigeni shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeshauriwa kuongeza idadi ya lugha za kigeni zinazofundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu nchini kwa lengo la kuwaandaa Watanzania kushirikiana na wawekezaji wa kigeni wanaowekeza nchini pamoja na kuwawezesha kufanya biashara za kimataifa.

Ushauri huo ulitolewana mbunge wa Lupa, Masache Kasaka wakati wa mahafari ya 33 ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mbalizi inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)

Alisema kwa sasa serikali inahamasisha wawekezaji wa kimataifa kuingia Tanzania na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali, hivyo ili kuwasaidia Watanzania kuajiriwa kwenye maeneo hayo ni lazima wafundishwe lugha za baadhi ya mataifa.

Vilevile alisema biashara baina ya Tanzania na baadhi ya mataifa hayo inakua kwa kasi kubwa na hivyo ili kuimarisha mawasiliano ni lazima Watanzania wajifunze lugha za mataifa hayo.

Alisema China ni miongoni mwa mataifa ambayo biashara yake na Tanzania inakua kwa kasi lakini asilimia kubwa ya raia wa nchi hiyo hawajui kiingereza wala Kiswahili.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mbalizi, Marco Shija alisema shule hiyo imeanzisha mikakati maalumu ya ufundishaji wa lugha mbalimbali za kigeni hasa kifaransa na kichina.

Alisema lugha hizo zinatumika zaidi duniani na hivyo inatakiwa Watanzania wengi wazijue lugha hizo ili kurahisisha mawasiliano ya kimataifa.

Hata hivyo alisema wameamua kuanza kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia TEHAMA ili kuhakikisha wanafunzi wanajifunza hata kwa njia ya mtandao.



# SMZ yapata mwarobaini kesi dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema maboresho yaliyofanywa na Mahakama Kuu ya Zanzibar yamefanikisha usikilizwaji wa kesi za dawa za kulevya kwa wakati baada ya kuongeza idadi ya majaji.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman wakati akizungumza na uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili, SMZ imefanya maboresho makubwa katika Idara ya Mahakama ikiwemo kuongeza idadi ya majaji kutoka wanane hadi kufikia 11 na mahakimu. Aliyataja maboresho mengine kuwa ni ujenzi wa mahakama za mwanzo na wilaya za visiwa vya Unguja na Pemba hadi kufikia 15.

"Maboresho makubwa tuliyoyafanya katika kipindi cha miaka miwili matunda yake yameonekana ambapo ni kuweza kusikiliza kesi kwa wakati na kutoa maamuzi," alisema.

Suleiman alisema walipatia ufumbuzi tatizo sugu la wananchi wa Kisiwa cha Pemba kupata Jaji mkazi wa kusikiliza mashauri kwa wakati.

"Tumekisikia kilio cha muda mrefu cha wananchi na viongozi wa Kisiwa cha Pemba kupata Jaji Mkazi ambaye kwa kiasi kikubwa atasikiliza kesi zinazohusu rufaa katika matukio mbalimbali, " alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Kanani Burhani Zubeir Nassor, alisema changamoto kubwa ya kuchelewa usikilizwaji kesi za dawa za kulevya ni pamoja na kupata matokeo ya vipimo vya uchunguzi wa madawa hayo kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na mashahidi.

Alisema wakati mwingine kesi imekaa vizuri kwa ajili ya kusikilizwa mahakamani, lakini tatizo ni kujitokeza mashahidi ambao wameshuhudia tukio hilo. "Yapo mambo mawili ambayo ni kikwazo katika usikilizaji wa kesi za dawa za kulevya ikiwemo kupata matokeo ya vipimo kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na jingine tatizo la kukamilika kwa ushahidi, wengine wanakataa na ndiyo maana kesi hizo zinachukua muda mrefu," alisema.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inaendelea kutekeleza majukumu yake baada ya mabadiliko ya sheria yaliyofanywa na Baraza la Wawakilishi kuwaongezea nguvu.

Katika marekebisho ya sheria yaliyofanywa na baraza hilo mwaka jana, mamlaka hiyo itakuwa na uwezo wa kukamata, kufanya uchunguzi na kufikisha mahakamani watuhumiwa kwa lengo la kuongeza kasi ya kusikiliza kesi hizo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Serengeti Breweries Ltd (SBL), Obinna Anyalebechi (kushoto), akikabidhi cheti kwa Ananastazia Koko ambaye ni mmoja wa wanufaika wa programu ya ufadhili wa masomo ya Kilimo Viwanda kutoka Chuo cha Kilimo cha Mtakatifu Maria Goretti cha Iringa, katika hafla iliyofanyika chuoni hapo jana. Wengine ni Mkurugenzi Mahusiano ya Umma wa SBL, John Wanyancha (wa pili kulia) na Mkuu wa chuo hicho, Isaya Kigava. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yaahidi ushirikiano bodi ya wahandisi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar imeahidi kuipatia ushirikiano bodi mpya ya wahandisi na wasanifu majengo kutimiza majukumu yao ya kazi.

Ahadi hiyo imetolewa na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Khalid Salum Mohamed wakati akizungumza na wajumbe wa bodi hiyo ofisini kwake jana.

Mohamed aliwahakikishia wajumbe hao kuwa wizara hiyo itashirikiana nao kuhakikisha changamoto zinazowakabili zinatatuliwa ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wao.

Dk. Khalid, alisema Serikali ipo katika utekelezaji wa ujenzi wa miradi mikubwa kwa gharama kubwa, hivyo wajumbe hao wanatakiwa kuwa makini kuwasimamia watendaji ili kufanikisha azma yake.

Kwa upande mwingine, Dk Khalid, aliwataka wajumbe hao kuweka mfumo maalumu wa utunzaji wa taarifa utakaosaidia kuwatambua wataalamu na kampuni zilizopo Zanzibar na kutoa uelewa wa kufuata taratibu za kujisajili kabla ya kuanza kazi zao.

Akizungumzia kuhusu upatikanaji wa wafanyakazi wa kudumu katika bodi hiyo, Katibu Mkuu Wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab, alisema wizara imeanza kuchukua hatua madhubuti kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Yasser De Costa, alisema wanafanyakazi kwa kuzingatia sheria na taratibu, hadi sasa imesajili wataalamu wapatao 843.

Alisema bodi hiyo ina mpango wa kutoa mafunzo kwa wataalamu wake ili kuwaelimisha namna bora ya usimamiaji wa majukumu yao ya kila siku.

# Makamu wa Rais akunwa ujenzi wa masoko Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Mbuzini Unguja.

Abdula aliwataka makandarasi na washauri elekezi kuongeza zaidi kasi ya ujenzi wa masoko hayo ili kukamilika kwa wakati na kwa ubora wa hali ya juu .

Alisema matarajio ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa masoko hayo yawe yamekamilika mwishoni mwa mwaka huu ili wafanyabiashara wayatumie kwa kujipatia kipato cha kila siku.

Makamu huyo wa Rais, alimshukuu Dk. Mwinyi kwa miongozo anayoitoa katika miradi hiyo na upatikanaji wa fedha kwa wakati na kuwapa moyo makandarasi wa kuongeza kasi ya ujenzi huo.

Alisema kuwa lengo la kujenga masoko hayo ni kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara na wananchi, usalama wa afya zao na kuepuka msongamano katika maeneo yasiyo rasmi.

Aliwaagiza wakurugenzi wa manispaa kuhakikisha wanatoa elimu na maelekezo kwa wafanyabiashara namna bora watakavyoyatumia masoko hayo na kuondoka pembezoni mwa barabara.

Abdula alisema Serikali imetumia gharama kubwa kujenga masoko hayo, hivyo umakini unahitajika katika kuyatumia na kuyatunza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Massoud Ali Moh'd, alisema ziara hiyo ya Makamu wa Pili wa Rais inaongeza hamasa ya kufanya kazi kwa ustadi wa hali ya juu ili kufiki malengo ya Serikali kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara.

Msanifu Majengo na Mshauri elekezi kutoka Wakala wa Majengo Zanzibar, Mhandisi Shadya Fauz Muhamed, alisema makandarasi wapo katika hatua za mwishoni kukamilisha ujenzi huo na vizimba vimeanza kujengwa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 129 OF 2023
In the matter of the Estate of the late
ASAN YOHANA MALUGU
of Mpunguzi within Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ALFERD ASSAN MALUGU

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 11,2023
Dated at Dodoma this 10 Day of 10, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

3FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.1101 OF 2023
In the matter of the estate of the late JUDITH MULOKOZI NYONYI
And
In the matter of Application for letters of administration by
JOSEPHINE NYONYI MAHAMBA

GENERAL CITATION
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters o administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 7 day of NOV 2023
Dated at DAR ES SALAAM this 17 day of October 2023

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA CHETI



**KURUTHUMU HASSAN MFAUME** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2656-0016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **FPCT-RUO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2020**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/MTW/NAN/435/2023**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 128 OF 2023
In the matter of the Estate of the late
BATHOLOMEO AMOS NHONO
of Mkonze within Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY
JULIANA BATHOLOMEO AMOS
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 11,2023
Dated at Dodoma this 10 Day of 10, 2023

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA
RESIDENT MAGISTRATE

MAHAKAMA YA WILAYA YA SINGIDA
MKOA WA SINGIDA
HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI
SHAURI LA MIRATHI NA 35/2023
OMBI LA CATHERINE JOSEPH LANGU KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU SIXTUS MTEE HUSEIN KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII

Watu wotu wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu **SIXTUS MTEE HUSEIN** wanaalikwa kuja mahakamani kuhudhuria kesi mnamo tarehe 09 mwezi 11 mwaka 2023, kabla mwombwji huyo hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Tarehe 19/10/2023
Hakimu mkazi
Mahakama ya Wilaya Singida

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YA MAGURUDUMU MATATU (TOYO)

**HAJI BAKARI KUBIHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki magurudumu matatu (TOYO) aina ya SINORAY yenye usajili namba MC 457 CXB, CHASSIS NAMBA: LZSHDNZG2M8002908 na ENGINE NAMBA: 163ML8M300062. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/28157/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THEOPHILUS STANILAUS KARUMUNA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDCRUISER DISCOVERY yenye usajili namba T 144 AEE , CHASSIS NAMBA: SALLJGMF7VA55789 na ENGINE NAMBA: 17119673A. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/4771/2023**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA
MBINGA
SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI NO. 3/2022
(Lililotokana na Shauri la gharama Na. 01/2022 Mahakama ya Wilaya Mbinga)
KATI YA
AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED..................MLETA MAOMBI
DHIDI YA
CHINA HENAN INTERNATIONAL CO OPERATION GROUP COMPANY LIMITED (CHICO LTD)......................MJIBU MAOMBI
KWA: CHICO LTD.

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe **01/11/2023** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la maombi ya utekelezaji tajwa hapo juu limepangwa kwaajili ya uamuzi mdogo.

Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **19/10/2023.**

A.A. MKAMA
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA
MBINGA
SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI NO. 3/2023
(Lililotokana na Shauri la Madai Na. 12/2022 Mahakama ya Wilaya Mbinga)
KATI YA
AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED..................MLETA MAOMBI
DHIDI YA
CHINA HENAN INTERNATIONAL CO OPERATION GROUP COMPANY LIMITED (CHICO LTD)......................MJIBU MAOMBI
KWA: CHICO LTD.

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe **01/11/2023** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la maombi ya utekelezaji tajwa hapo juu limepangwa kwaajili ya uamuzi mdogo.

Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **19/10/2023.**

A.A. MKAMA
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
P.O.BOX 11


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ARNOLD GAMALIEL MWANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TATA LPT TRUCK yenye jina la umiliki PROGRESSIVE GENERAL LTD TANZANIA yenye usajili namba: T 920 BXS, CHASSIS NAMBA: MAT450020B7R40061 na ENGINE NAMBA: BS91002011G63159836. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/IRI/IRI/2239/2023**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP. 117) R.E 2019**
**CHANGE OF NAMES BY DEED POLL**

BY THIS DEED, LETICIA CHACHA TUMAINI of P.O.BOX 219 BUNDA, MARA formally known as LETICIA TUMAINI CHACHA do hereby wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of the names LETICIA TUMAINI CHACHA which are appearing on my NATIONAL IDENTITY CARD with No 1997020 567129 00002 11.
IN PURSUANCE of such changes of name as aforesaid, I HEREBY DECLARE that I shall, at all times hereafter and in all records, deed and instruments in writing and in all actions, proceedings, dealings, transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the said names of LETICIA CHACHA TUMAINI which are appearing on my CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION, CERTIFICATION OF BIRTH and ADVANCED CERTIFICATION OF SECONDARY EDUCATION lieu of LETICIA TUMAINI CHACHA the names herein above renounced and abandoned.
FOR THAT REASON, I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST all persons to designate and address me in the names of LETICIA CHACHA TUMAINI IN WHITNESS WHEREOF I have hereunto set my hand at Bunda this 12 day of September 2023.

SIGNED and DELIVERED by
LETICIA CHACHA TUMAINI
who is known to me personally
this 12 day of September 2023 LETICIA CHACHA TUMAINI
BEFORE ME:
NAME GODFREY MAHOBHE MUROBA
SIGNATURE
POSTAL ADDRESS P.O.BOX 201 BUNDA, MARA
QUALIFICATION COMMISSIONER FOR OATHS



## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DANIEL PHILIMON MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki KISHEN ENTREPRISES LTD usajili namba T781 CVD, CHASSIS NAMBA: KE7KEFPK013583 na ENGINE NAMBA: 162FMJD5176568. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/4116/2023**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Msafara wa malori yaliyosheheni misaada ya kibinadamu kutokea Misri ukisubiri kupewa ruhusa ya kupita kivuko cha Rafah tayari kuelekea Gaza. **PICHA: REUTERS**

# Misaada yaruhusiwa kuingia Gaza, Israel yatoa onyo Hamas wasiguse

**TEL AVIV, Israel**

ISRAEL imetangaza kuruhusu misaada ya kiutu kuingia Ukanda wa Gaza kutokea nchini Misri baada ya kulizingira eneo hilo kwa wiki mbili tangu kutokea kwa shambulio lililofanywa na wanamgambo wa Hamas.

Ofisi ya waziri mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu ilisema katika taarifa yake ya jana kuwa uamuzi huo wa baraza la mawaziri umetokana na maombi ya Rais wa Marekani Joe Biden.

Taarifa hiyo ilisisitiza kwamba misaada ya kiutu itakayoruhusiwa ni ile itakayokwenda kwa raia walioko kusini mwa Gaza.

Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus amekaribisha tangazo hilo na kusema kwamba maisha ya watu wengi yanategemea uamuzi huo.

Raia wa Gaza wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa mahitaji ya msingi baada ya eneo hilo kuzingirwa na majeshi ya Israel kufuatia shambulizi la kushtukiza la Hamas ndani ya nchi hiyo na kuua Waisraeli wapatao 1400 na maelfu kujeruhiwa.

Rais wa Marekani, Joe Biden alilikaribisha tangazo hilo kwa furaha na amesifu ziara yake ambayo pia ameahidi msaada wa Dola milioni 100 kwa Wapalestina huko Gaza na Ukingo wa Magharibi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Biden alisema watu wa Gaza wanahitaji chakula, maji, madawa na malazi.

Rais huyo amekiri kwamba misaada inayoingia Gaza itapekuliwa na haitopaswa kuwafikia Hamas, bila kutoa ufafanuzi ikiwa analenga tawi la wapiganaji, viongozi wa kisiasa au wizara za serikali zinazoendeshwa na kundi hilo.

Wakati wa ziara yake nchini Israel, Biden aliahidi msaada wa kijeshi kwa nchi hiyo katika kuhakikisha kwamba mfumo wake wa ulinzi wa angani Iron Dome unaendelea kufanya kazi.

Juzi, Marekani ilipinga azimio la Umoja wa Mataifa la kulaani ghasia katika vita vya Israel na Hamas, ikisema ni mapema mno kuandaa azimio mwafaka la Baraza la Usalama katika mgogoro huo.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa Linda Thomas-Greenfield alisema baraza hilo linahitaji kuruhusu juhudi za sasa za kidiplomasia na kutafuta ukweli zaidi wa kile kinachoendelea.

Balozi huyo pia alikosoa hatua za kushindwa kusisitiza haki ya Israel kujilinda.

Azimio hilo lililoandaliwa na Brazil lilikuwa na uungwaji mkono mkubwa na limelaani ghasia zote dhidi ya raia, ikiwa ni pamoja na mashambulio ya Hamas dhidi ya Israel.

Wakati huo huo uongozi wa Palestina ulisema kuwa kitendo cha kuwahamisha raia kinguvu kutoka ukanda wa gaza ni kuvuka mstari mwekundu na haitoruhusu hilo kutokea.

Taarifa hiyo ilitolewa baada ya viongozi kukutana mjini Ramallah.

Katika hatua nyingine maelfu ya raia katika nchi za Kiarabu na Kiislamu duniani waliandamana kupinga vifo vya mamia ya watu katika shambulizi lililofanywa katika hospitali mjini Gaza na kuishutumu moja kwa moja Israel licha ya kwamba imekana kuhusika.

Hata hivyo, Israel na Hamas wametupiana lawama kuhusu shambulio hilo, huku jeshi la Israel likisema baadaye lilikuwa na ushahidi kwamba walikuwa wanamgambo walihusika.

Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak amewasili nchini Israel na kuwaambia waandishi wa habari katika uwanja wa ndege wa Tel Aviv kwamba mashambulizi ya Hamas ya Okoba 7, lilikuwa tukio la kigaidi lisiloelezeka.

Alisisitiza kwamba Uingereza inasimama pamoja na Israel.

"Nasubiri sana mikutano yangu baadaye na waziri mkuu na rais na ninatumaini itakuwa mikutano yenye tija," alisema Sunak.

Jeshi la Israeli limeongeza idadi ya watu wanaojulikana kuwa wameshikwa mateka katika shambulio la Oktoba 7, na kufikia 203.

Msemaji wa Jeshi la Israel (IDF), Daniel Hagari alisema jeshi limefahamisha familia za mateka wote wanaoshikiliwa ukanda wa Gaza.

Mashambulio ya mabomu ya Israel yanaendelea katika Ukanda wa Gaza, hususan maeneo ya kaskazini, huku mashambulizi yaliyotekelezwa alfajiri ya Alhamisi yakiharibu minara miwili katika jumba la Al-Zahraa Towers kwenye Ukanda huo katika Jimbo la Kati.

Mlipuko huo pia ulijumuisha kambi ya Jabalia na Nuseirat.

Makumi ya wakaazi wameuawa katika uvamizi wa leo kwenye maeneo tofauti ya Gaza, kulingana na Shirika la Habari la Palestina.

Vyanzo vya habari vya ndani viliripoti kuwa ndege za Israel zilivamia nyumba za raia huko Khan Yunis na Rafah, na kupata miili 30 ya wanafamilia wanaoishi katika eneo hilo, na idadi kubwa ya wakaazi walijeruhiwa na kupelekwa katika Hospitali ya "Martyr Abu Youssef Al-Najjar".

Idadi kamili ya Wapalestina waliouawa kutokana na mashambulizi ya Israel wakiwa kwenye nyumba zao huko Gaza pamoja na watoto bado haijajulikana huku watu wengine wakipotea chini ya vifusi.

**DW**

# Uganda yawashutumu ADF kuwaua wanandoa

**KAMPALA, Uganda**

UGANDA imelishutumu kundi la waasi wa ADF kuhusika kuwauwa wanandoa raia wa Afrika Kusini na Uingereza wakati walipokwenda kutalii katika Mbuga ya Wanyama ya Malkia Elizabeth II.

Wanandoa hao David na Celia Barlow, wanatoka Norreys, karibu na Newbury huko Berkshire.

Polisi wa Uganda walisema gari lao lilichomwa moto baada ya kuuawa.

Kundi la ADF, ambalo lilianzisha uasi nchini Uganda na limekuwa likiendesha shughuli zake katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo tangu mwishoni mwa miaka ya 1990, lilitangaza utiifu kwa kundi la Dola la Kiislamu (IS) miaka minne iliyopita.

**BBC**

# China yasifu mradi kuunganisha dunia

**BEIJING, China**

RAIS wa China Xi Jinping amesema mradi mkubwa wa miundombinu ya barabara na reli, BRI uko katika njia sahihi licha ya kuibuka kwa mivutano na mizozo ya kimataifa.

Kulingana na rais Xi Jinping, mataifa yanayoendelea yanatakiwa pia kunufaika na mradi huo wa miundombinu ya barabara na reli ulioanzishwa miaka 10 iliyopita.

Akizungumza mbele ya wawakilishi wa nchi 140 duniani kote akiwemo Rais wa Russia, Vladimir Putini, alisema mabadiliko ya kihistoria yanaonekana ulimwenguni kote.

Kwenye hotuba yake, Rais Xi aliikosoa Marekani na mataifa ya Umoja wa Ulaya kama Ujerumani ambayo si wanachama wa mradi huo kwa kuwekea vikwazo taifa hilo au kuzichunguza bidhaa zake na kuongeza kuwa vikwazo hivyo vya upande mmoja vinazuwia ukuaji wa kiuchumi na kuvuruga mifumo ya ugavi.

**DW**

**Akizungumza mbele ya wawakilishi wa nchi 140 duniani kote akiwemo Rais wa Russia, Vladimir Putini, alisema mabadiliko ya kihistoria yanaonekana ulimwenguni kote.**

# KMC YAPANGA KUENDELEZA DOZI IKIWAVAA TABORA UTD

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inajiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, benchi la ufundi la KMC FC limesema limejipanga imara kuhakikisha linazibeba pointi tatu muhimu katika mchezo wao dhidi ya Tabora United utakaopigwa keshokutwa.

Mechi hiyo imepangwa kufanyika kuanzia saa 10:00 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani Tabora.

KMC FC itashuka dimbani ugenini ikihitaji kuendelea kusaka ushindi baada ya kushinda michezo mitatu iliyopita.

Timu hiyo ya Halmashauri ya Kinondoni ilifanikiwa kushinda mechi mbili za nyumbani wakicheza dhidi ya JKT Tanzania kuwapa kichapo cha mabao 2-1, iliwafunga Ihefu bao 1-0 na ikaenda kushinda ugenini dhidi ya Geita Gold FC mabao 2-1.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moalini alisema wamefanya maandalizi mazuri na wako tayari kwa ajili ya kupata matokeo chanya katika mchezo huo.

Moalim alisema anafahamu ugumu wa ligi na kila timu imefanya maandalizi mazuri na wachezaji wake wako tayari kupambana kuvuna pointi tatu ili kuendelea kujiimarisha katika msimamo.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu Tabora United wamejiandaa vizuri, tunaenda kukutana na wapinzani wetu kwa tahadhari na heshima kubwa kwa sababu malengo yetu ni kusaka pointi kila mechi," alisema Moalin.

Aliongeza amefanyia kazi changamoto za mechi iliyopita na anaimani vijana wake watafuata maelekezo aliyowapatia katika uwanja wa mazoezi na kuonyesha kwenye mchezo huo.

Simba yenye pointi 15 ndio vinara katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali wakati Yanga ndio mabingwa watetezi.




Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya 'Music In Africa Foundation' Eddie Hatitye akizungumza na waandishi wa habari jana juu ya msimu wa pili wa tamasha la muziki la Access litakalofanyika jijini Dar es Salaam mwezi ujao, kulia na Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# BMT yasimamisha uchaguzi TEFA

**Na Saada Akida**

UCHAGUZI mdogo wa Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Temeke (TEFA), umesogezwa mbele hadi hapo itakapotafangazwa tena, imeelezwa.

Baraza la Michezo la Taifa (BMT), limesimamishwa uchaguzi huo ambao awali ulitarajiwa kufanyika keshokutwa.

TEFA ilipanga kufanya uchaguzi wa kuziba nafasi ya aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Peter Mhinzi, ambaye alifariki dunia.

Akizungumza na Nipashe jana, Msajili wa Vyama vya soka nchini, Evordy Kyando alisema wamepokea barua kutoka wa wanachama wa TEFA wakidai waliingiliwa katika mchakato wa uchaguzi huo na mabosi wa Chama cha Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA) na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Alisema baada ya kufuatilia malalamiko ya wanachama hao, BMT ilifanya mazungumzo na viongozi wa TEFA, DRFA na TFF ili kupata ukweli.

"Kwa sababu muda ulikuwa mdogo kupitia vielelezo vya pande zote mbili, tunaona tuchukue uamuzi mdogo wa uchaguzi huu kutofanyika kwa siku hiyo ya Jumapili hadi hapo tutakapopitia kwa uyakinifu vielelezo vyote.

Tunahitaji kila mmoja kupata haki zake katika hili," alisema Kyando.

Alisema BMT ilipokea barua ya malalamiko kutoka kwa wadau Oktoba 13, mwaka huu na sasa itapitia kila nyaraka na baadaye itatangaza siku nyingine ya kufanyika kwa uchaguzi huo.

## Beting yaingiza mapato bil 170.4/-

**Na Faustine Feliciane**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) imesema katika kipindi cha fedha cha mwaka 2022/2023 imechangia pato la taifa la Sh. bilioni 170.4 zilizotokana na makusanyo mbalimbali katika shughuli zake zikiwamo ada za makampuni ya kubashiri michezo 'Beting'.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuekea maadhimisho ya miaka 20 tangu kunzishwa kwake, Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe alisema bodi hiyo imepata mafanikio makubwa ukilinganisha na miaka ya nyuma ilipoanzishwa.

Mbalwe alisema kuingia kwa makampuni ya kubashiri matokeo ya michezo mbalimbali kumechangia kupata makusanyo makubwa ndani ya GBT.

"Wakati tunaanza hali ilikuwa ngumu, hakukuwa na makampuni ya kubashiri michezo hivyo hata makusanyo hayakuwa makubwa, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006/2007 tulikuwa tukikusanya shilingi bilioni 2.8 tu," alisema Mbelwa.

Mkurugenzi huyo alisema kuingia kwa makampuni hayo ya kubashiri mwaka 2013 mapato yalianza kuongezeka zaidi na mpaka mwaka wa fedha wa 2022/2023 walifanikiwa kukusanya kiasi hicho cha Sh. bilioni 170.4.

"Haya ni mafanikio makubwa sana, fedha hizi tumekusanya mwaka wa fedha uliopita tu (2022/2023), na kufanikiwa kuchangia pato letu la taifa, fedha nyingi zimetokana na kodi na ada za makampuni ya kubeti," alisema Mbelwa.

Aliongeza wanatarajia kuona makusanyo ya kodi na ushuru mwingine yakiongezeka miaka inayofuata hasa kutokana na uwepo wa makampuni mengi yanayojihusisha na michezo ya bahati nasibu na kubashiri.

"Wakati bodi hii inaanza kazi zake mwaka 2003 hakukuwa na makumpuni ya kubashiri michezo, kulikuwa na michezo mitatu tu, na mpaka tunafika mwaka 2006 kulikuwa na makampuni 23 tu ambayo yalikuwa yanaendesha michezo hii.

Sasa hivi tunavyoongea mwaka 2023 kuna makampuni zaidi ya 100 tuliyoyasajili kuendesha michezo hii, tunaamini idadi hii inaweza kuongezeka," Mbelwa aliongeza.

Alisema mchango wa sekta katika maendeleo ya jamii umekuwa mkubwa ambapo ajira ziliongezeka kutoka watu 600 katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na kufikia wafanyakazi 25,000 kwa mwaka wa fedha uliopita.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OSIMHEN AWINDWA**
LIVERPOOL imeungana na Chelsea na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsaka mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, ambaye anakadiriwa kuwa pauni milioni 95. **(Sun)**

**MESSI NA TETESI**
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 36 amepuuza tetesi kwamba ataondoka Inter Miami kwa mkopo kwenda kuchezea klabu nyingine mara tu msimu wa MLS utakapomalizika. **(ESPN)**

**SUAREZ KUTUA MIAMI**
INTER Miami inatarajia kumsajili mshambuliaji wa Uruguay na Gremio, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 36 kwenye klabu hiyo ili kuungana na mchezaji mwenza wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi. **(Mirror)**

**SILVA KUREJEA**
MLINZI wa Chelsea Mbrazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 39 amedokeza kurejea Fluminense mwakani, huku mkataba wake na The Blues ukitarajiwa kukamilika msimu huu wa majira ya joto. **(Sun)**

**PAPASTATHOPOULOS AWANIWA**
KLABU ya Bayern Munich inapania kumnunua mlinzi wa zamani wa Arsenal, Mgiriki Sokratis Papastathopoulos mwenye umri wa miaka 35. **(Mirror)**

**KONE AGOMBEWA**
KLABU ya Borussia Monchengladbach imeanzisha chaguo la kuongeza mkataba kwa kiungo wa kati wa Ufaransa, Manu Kone huku Liverpool, Juventus na Bayern Munich wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. **(90 min)**

**BONIFACE KUTUA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Nigeria, Victor Boniface mwenye umri wa miaka 22. **(Sun)**

**MUSIALA KUSAINI**
BAYERN Munich ina uhakika wa kumsainisha kiungo wa kati wa Ujerumani, Jamal Musiala kwenye mkataba mpya huku Liverpool na Manchester City zikiwa na nia ya kumsajili ingawa mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 unaendelea hadi 2026. **(90 min)**

**CANIO ALIKATALIA MANCINI**
NYOTA wa zamani wa West Ham, Paolo Di Canio mwenye umri wa miaka 55 amefichua kuwa alikataa nafasi ya kujiunga na safu ya kocha Roberto Mancini katika timu ya taifa ya Saudi Arabia. **(La Stampa, via Sun)**

**JEWELL NA BRIGHON**
KLABU ya Rangers imemwendea mkuu wa uajiri wa Brighton, Sam Jewell, ambaye yuko nyuma ya wachezaji wakubwa waliosajiliwa na Seagulls. **(Star)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR NJE YA UWANJA MIEZI NANE

**Baada ya kupasuka goti lake kwenye majukumu ya timu yake ya taifa, kufanyiwa....**

**SAO PAULO, Brazil**

NYOTA wa Brazil, Neymar atalazimika kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu baada ya vipimo kuthibitisha kuwa alipasuka goti lake la kushoto wakati timu yake ya taifa ililipofungwa na Uruguay kwenye mechi ya kufuzu kombe la Dunia, shirikisho la soka la Brazil, CBF, lilitangaza jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 atafanyiwa upasuaji katika tarehe itakayotangazwa baadae.

Vyanzo viliiambia ESPN Brasil kwamba Neymar anaweza kurudi uwanjani baada ya miezi nane.

"Mshambuliaji Neymar Jr wa timu ya Brazil na Al-Hilal, kutoka Saudi Arabia, alifanyiwa vipimo vya kiafya, ambavyo vilithibitisha kupasuka kwa goti lake la kushoto," taarifa ya shirikisho la soka la Brazil lilisema.

"Mshambuliaji huyo atafanyiwa upasuaji katika tarehe ambayo bado haijatajwa ili kurekebisha goti lake. Idara ya matibabu ya timu ya Taifa ya Brazil chini ya usimamizi wa Dk. Rodrigo Lasmar, na Al Hilal, wana mawasiliano ya kudumu na wamejipanga katika kupona haraka kwa mchezaj," lilisema Shirika hilo.

Baadaye Jumatano, Neymar alisema katika ujumbe kwenye kurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram "nina nguvu" lakini atahitaji usaidizi mkubwa ili kurejea uwanjani.

"Ni wakati wa kusikitisha sana, mbaya zaidi," aliandika Neymar.

"Najua nina nguvu lakini wakati huu nitahitaji familia yangu na marafiki zaidi. Si rahisi kupitia jeraha na upasuaji. Hebu fikiria kupitia tena baada ya miezi 4 ya kupona," alisema Neymar.

Al Hilal ilituma salamu za heri kwa Neymar na kutuma picha kwenye mitandao ya kijamii ya nyota huyo wa Brazil alipokuwa akitolewa nje ya uwanja na ujumbe.

Neymar alijikwaa na kuanguka wakati wa kukimbia katika dakika ya 44 ya mchezo huo ambao Brazil ililala kwa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Centenario na mara moja alizingirwa na wachezaji wa timu zote mbili huku akishikilia goti lake la kushoto.

Mshambliajii huyo wa zamani wa Barcelona na PSG alibebwa nje kwa machela huku akiweka mikono yake usoni, huku mchezaji mwenzake Richarlison akichukua nafasi yake.

Neymar, ambaye ni mfungaji bora wa muda wote wa wanaume wa Brazil akiwa na mabao 79 katika mechi 129, hivi majuzi alipona jeraha baya la kifundo cha mguu wa kulia.

# JINA LA MESSI LAVUJA BALLON D'OR



**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi anatarajia kushinda tuzo ya nane ya Ballon d'Or baadae mwezi huu baada ya majina ya washindi kwa upande wa wanaume na wanawake wa tuzo za mwaka huu wa 2023 kuvuja.

Messi mwenye umri wa miaka 36, ameonekana kushinda baada ya kuiwezesha Argentina kushinda ubingwa wa Kombe la Dunia 2022 katika fainali zilizofanyika huko Qatar mwaka jana.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Barcelona na Paris Saint-Germain alijiunga na Inter Miami, Julai mwaka huu na tangu wakati huo amekuwa moto kwenye ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS.

Baada ya kukosa tuzo ya mwaka 2022 iliyonyakuliwa na Karim Benzema, Messi anaripotiwa kwamba atanyakua tuzo hii ya mwaka huu, ambayo sherehe yake itafanyika jijini Paris, Ufaransa, Jumatatu ya Oktoba 30.

Messi akishinda basi atakuwa mchezaji wa kwanza kushinda Ballon dOr akiwa nje ya Ulaya na hapo atakuwa ameweka pengo la tuzo tatu dhidi ya mpinzani wake Cristiano Ronaldo.

Na kwenye kinyang'anyiro cha mwaka huu, Messi anaripotiwa kumpiku straika wa Manchester City, Erling Haaland na mchezaji mwenzake wa zamani wa PSG, Kylian Mbappe.

Haaland alishinda mataji matatu akiwa na kikosi cha Man City mwaka jana baada ya kufunga mabao 52 katika mechi53.

Wakati Mbappe, alifunga hat-trick kwenye fainali ya Kombe la Dunia walipokabiliana na Argentina ya Messi na alifanya vizuri alipokuwa na kikosi cha PSG, lakini Messi amekuwa na nafasi kubwa ya kushinda baada ya kuipa Argentina ubingwa wa Kombe la Dunia na alifunga mabao muhimu katika michuano hiyo.

# Lingard kutimkia Saudi Arabia

**LONDON, England**


MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Jesse Lingard anakaribia kusaini katika klabu ya Al Ettifaq mara ya nchini Saudi Aarabia baada ya muda wake wa kutazamwa mwenendo wake kwenda vizuri.

Klabu hiyo inanolewa na nahodha wa zamani wa England na Liverpool, Steven Gerrard imeweka wazi kuwa msimu ujao watakuwa na Lingard baada ya kuridhishwa na maendeleo yake.

Gerrard anataka kumsajili Lingard lakini itabidi asubiri hadi mwezi Januari kutokana na sheria za kusajili wachezaji wa kigeni nchini Saudi Arabia kubana kwa sasa.

Wachezaji wa kigeni Saudi wanapaswa wasizidi 8 kwenye orodha wa wachezaji wanaocheza mechi na hadi sasa Al Etifaq ina wachezaji 10 wa kigeni.

Kwa mantiki hiyo kuna namna ambavyo klabu hiyo itawatoa baadhi ya wachezaji ili wapitishe jina la Lingard.



# Ancelotti aikataa Brazil



**MADRID, Italia**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amekanusha taarifa za kwenda kuitumikia timu ya Taifa ya Brazil msimu ujao.

Ancelotti amesema hizo ni tetesi tu na yeye anafurahia kuwa pale katika Klabu ya Real Madrid.

Malengo yake ya sasa na msimu ujao ni kuwapa mataji Madrid kama ambavyo amekuwa akifanya mara kadhaa.

Carlo ambaye anatajwa kuwa ndiye kocha mwenye mafanikio makubwa zaidi duniani, amesema kuinoa timu kama Brazil ni ndoto ya kila kocha, lakini kwake yeye anaona bado kwa sasa.

"Nafikiri hizi ni taarifa kama ambavyo imekuwa kawaida kwa wachezaji na makocha kwenye soko la mpira Duniani. Nafurahia kuwepo Madrid.

"Nafurahia kufanya kazi kwenye klabu kubwa na yenye mafanikio makubwa Duniani. Sijui kuhusu jambo lingine kwa sasa," amesema.

Ikumbukwe hivi karibuni taarifa zilitoka kuwa Ancelotti tayari amesaini mkataba wa kuinoa Brazil na msimu ujao hatokuwa na Madrid.

# ZAHERA MAMBO MAGUMU COASTAL UNION, ATOWEKA

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Mwinyi Zahera inadaiwa yupo katika kitimoto, huku klabu yake ikitarajiwa kutoa uamuzi kuhusiana na hatima yake.

Uamuzi huo umetokana na mwenendo wa kutoridhisha wa timu hiyo tangu kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/2024.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abass El Sabri alisema mabosi wa klabu hiyo walikuwa na kikao 'kizito' usiku wa kuamkia jana ambacho kilijadili mwenendo mbaya wa timu yao na baada ya kumalizika kwa kikao hicho, wanatarajia kutoa tamko rasmi.

Hata hivyo, habari kutoka ndani ya kikao zinasema Zahera ana asilimia kubwa ya kutimuliwa kutokana na uongozi kutoridhishwa na kiwango cha timu ambayo hadi sasa imevuna pointi mbili kutoka katika mechi tano walizocheza.

Habari zinasema kocha hayupo na timu, na kwa sasa mazoezi ya kikosi chao yanasimamiwa na Kocha Msaidizi, Fikiri Elius wakisaidiwa na wachezaji wawili wa zamani wa timu hiyo, Abdallah Sabebe na Razack Yusuph 'Careca.'

"Kikao kiliisha usiku mzito wa kuamkia jana (juzi), lengo ilikuwa ni kwa nini Coastal Union ipo mkiani, kwa nini malengo yetu mpaka kufikia raundi ya tano bado hajaonekana na yanazidi kutia shaka, maana kwa mechi tano tulitakiwa kuwa na angalau nusu ya pointi 15, lakini mechi tano, mkononi tuna pointi mbili, hii haikubaliki.

Coastal Union ni moja kati ya timu ambazo hazijashinda mechi hata moja ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa sawa na Mtibwa Sugar ambayo tayari imeshatangaza kuachana na kocha wake, Habib Kondo na taarifa zinamtaja, Zuberi Katwila anaweza kurejea katika kikosi hicho cha Manungu.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa kuwavaa Botswana katika mechi ya kufuzu Michezo ya Olimpiki itakayochezwa Oktoba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA:TFF**

## Gamondi, Dabo watambiana

INATOKA UK. 24

natarajia mechi itakuwa nzuri, mgumu na ya kipekee, lakini sisi kama Yanga tumejipanga kushinda," alisema.

Kocha Mkuu wa Azam, Dabo kwa upande wake amewataka wachezaji wake wacheze mechi hiyo kulingana na tathamani na uwezo wao na si tu kwamba wanakwenda kucheza dhidi ya Yanga.

"Tulicheza na Yanga kule Tanga, nimewaona, kwa hiyo sitaki wachezaji wangu waende uwanjani wakiwa na presha kwa sababu tunacheza na Yanga," alisema Dabo.

Alisema kwenye mechi dhidi ya Yanga anatarajia kuona mabadiliko ya kiuchezaji kwa wachezaji wake baada ya kukaa nao na kuwambia mambo kadhaa wanayopaswa kufanya na wataingia uwanjani wakiwa tofauti kulinganisha na mchezo wa mwisho kukutana.

"Nimeshawaambia wachezaji wangu wasicheze mechi kwa bidii kwenye baadhi ya michezo tu, tunapaswa kucheza kwa nguvu na bidii katika michezo yote, kila mpinzani tunayepambana naye tunapaswa kucheza kwa kiwango kile kile, tunatakiwa kila mechi tucheze kwa ajili ya kupata ushindi, " alisema kocha huyo raia wa Senegal.

# Nassib atamba kumchapa Batyi

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Nassib Ramadhan ametamba kumchakaza mpinzani wake, Zolisa Batyi kutoka Afrika Kusini katika pambano lisilokuwa la ubingwa litakalofanyika Oktoba 28, mwaka huu kwenye Ukumbi wa PTA, Dar es Salaam.

Akizungumza Nipashe jana, Ramadhan alisema anaendelea vyema na maandalizi kuelekea pambano hilo na anaamini ataibuka na ushindi na hatimaye kupata mchezo mwingine.

Alisema amemfuatilia mpinzani wake na kufahamu ni bondia mzuri, lakini ameona ubora na madhaifu yake ambayo anayafanyia kazi ili afikie malengo.

"Mpinzani wangu yuko vizuri na natakiwa kujiandaa vizuri ili kukabiliana naye, ninataka kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania, sitaki kuona napata aibu kwenye ardhi ya nyumbani kwangu kwa kupigwa.

Nimepanga kumaliza pambano hili mapema kabla ya kufikia raundi hiyo ya 10, nawaomba mashabiki na wadau wa ngumi wajitokeze kwa wingi kushuhudia, niko tayari na nimejiandaa vizuri," alitamba bondia huyo.

## Simba yapania kuiheshimisha

INATOKA UK. 24

kwenye safu ya ulinzi akuiungana pia na Mohamed Hussein na Shomari Kapombe.

Kwa upande wake Nahodha wa Simba, John Bocco alisema mchezo huo kwao ni muhimu kutokana na kuchezwa mbele ya mashabiki wao lakini pia ni nafasi nzuri kwa wachezaji kujitangaza kimataifa..

Alisema wanaenda kuonyesha mchezo wa kiungwana na wanaimani Al Ahly ni timu kubwa lakini wamejipanga kupata matokeo mazuri katika uwanja wa nyumbani.

"Mchezo utakuwa mgumu, tunaamini maandalizi yalikuwa mazuri na tuko tayari kukutana na wapinzani wetu, tutahakikisha tunawapa furaha mashabiki na kuipa heshima klabu na Nchi kwa sababu ni mara ya kwanza mashindano haya yanafanyika na tumepata bahati ya kushiriki na mchezo wa ufunguzi kufanyikia hapa kwetu," alisema Bocco.

Kocha wa Al Ahly, Marcel Koller, alisema kuwa wanafuraha kucheza mchezo wa kwanza wa ufunguzi ingawa anaamini utaenda kuwa mchezo mgumu.

"Ninajua kuwa Al Ahly amepoteza mara mbili hapa nimekuja kubadili historia hiyo ingawa tunaenda kucheza na timu bora Afrika, nina mwaka mmoja tu kwenye klabu (Al Ahly) hivyo historia itabaki ila tumekuja kupata matokeo," alisema Koller na kuongeza,

"Sio rahisi kuandaa timu kwa siku mbili wachezaji wangu baadhi walikuwa kwenye majukumu ya mataifa yao, lakini naamini kwenye uzoefu wa wachezaji wangu, naamini tutaenda kupata matokeo mazuri, tunafahamu Simba ni imara sana wakiwa nyumbani.."alisema Koller.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro alisema Serikali imejipambanua katika kuendelea michezo kwa manufaa ya nchini, klabu na wachezaji.

Alisema wanatumia mchezo huo kujiweka kwenye ramani ya soka kama nchi na kuandika historia kwa sababu ni mara ya kwa kwanza kuanzishwa kwa mashindano hayo na mchezo wake wa ufunguzi kufanyika Tanzania.

"Sasa hivi wageni wako wengi tunapokea Marais 54 wa mashirikisho ya soka barani Afrika na ujio huu utanufaisha kila mtu hapa nchini na kuwainua kiuchumi, mechi hii sio ndogo, ukiangalia Simba ni timu ya saba unakutana na timu iliyokuwa ya kwanza katika msimamo wa Afrika. Hii mechi kwa wachezaji wa Simba ni kipimo tosha cha kuona ubora wao.

"Lakini pia unaona jinsi gani mashindano haya yalivyombeba kila mtu kwa sababu msanii wa Tanzania Ally Kiba atakuwa sehemu ya kuwapa burudani ya muziki kwa wageni watakashuhudia mchezo huo," alisema Ndumbaro.

Aliongeza kuwa Tanzania imepata heshima nyingine kwa mchezo wa TP Mazembe dhidi ya Esperance wa mashindano hayo kuchezwa hapa nchini katika uwanja wa Benjamin Mkapa keshokutwa Jumapili.

Michezo
Ijumaa Oktoba 20, 2023
Nipashe



**Jina la Messi lavuja Ballon d'Or**

UKURASA 22

## AFRICAN FOOTBAL LEAGUE..

# SIMBA YAPANIA KUIHESHIMISHA NCHI LEO

●●●Robertinho aita mashabiki uwanjani, asema ahadi ya Rais Samia imewaongezea mzuka wachezaji, Afrika yote jicho kwa Mkapa....



Perci Tau



Miquissone

**Na Saada Akida**

SIKU ambayo ilikuwa ikisubiriwa na wadau wengi wa soka Barani Afrika imefika ambapo leo wawakilishi wa Tanzania na Afrika Mashariki klabu ya Simba itaumana na wawakilishi wa Afrika Kaskazini na mabingwa wa Misri, Al Ahly kwenye mchezo wa ufunguzi wa michuano ya African Football League.

Mchezo huo wa michuano hiyo utaanza saa 12:00 jioni na kushuhudiwa na viongozi wakubwa wa soka Afrika na Duniani kwa ujumla.

Tanzania imepata bahati ya kuzindua mashindano haya yanayoshirikisha timu nane, Al Ahly, Mamelodi Sundowns, Esperance, TP Mazembe,Wydad Casablanca, Petro Atletico, Enyimba na Simba ambapo bingwa wa michuano atajishindia kiasi cha dola milioni nne ambazo ni sawa na Shilingi bilioni 10 za kitanzania .

Timu hizo kwa sasa zinakutana kwa mara ya pili kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa ndani ya kipindi cha miaka minne ambapo katika mechi zote Simba iliibuka na ushindi wa bao 1-0 katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2019 na 2021.

Kocha wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema hakuna sababu ya kuwafanya washindwe kuibuka na ushindi kwenye mchezo wa leo na amewataka mashabiki wa timu hiyo kufurika kwa wingi uwanjani kuwapa hamasa wachezaji wao.

"Tunawaheshimu Al Ahly kutokana na mafanikio yao kwenye soka la Afrika, lakini hiyo sio sababu ya sisi kushindwa kufanya vizuri, tumejiandaa vizuri wachezaji wangu wapo katika hali nzuri ya kiushindani hasa tukiamini tunacheza mbele ya maelfu ya mashabiki wetu," alisema Robertinho.

Aidha, alisema ahadi iliyotolewa na Rais wa Sami Suluhu Hassan ya kuzawadia shilingi milioni 10 kwa kila bao watakalofunga limeongeza hamasa kwa wachezaji wake.

"Wachezaji wangu hamasa imeongezeka, nafahamu mpira wa miguu unakuwa na matokeo ya kushangaza, lakini nina uhakika wa kufanya vizuri kwenye mchezo wa kesho," alisema Robertinho.

"Sina presha na mchezo wa kesho (leo) licha ya ukubwa wa mchezo, hata mimi nikiwa mchezaji kule Brazil nimewahi kukutana na mechi kama hizi kwenye Uwanja wa Maracana, kwa hiyo naifurahia na sina presha," aliongeza kusema Robertin.

"Ni kweli tunacheza mechi kubwa, Al Ahly ni timu bora na ina uzoefu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini kwangu mpira ni sanaa sio vita tunaenda kuonyesha ukubwa wetu na tupo tayari kwa dakika 90 za kesho (leo)," alisema Robertinho.

Robertinho alisema amefurahishwa zaidi kurejea kwa beki wake wa kati, Henock Inonga ambaye atamtumia kwenye mchezo wa leo akicheza pamoja na Che Malone

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi, Dabo watambiana

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Mabingwa Watetezi, Yanga, dhidi ya Azam FC iliyokuwa ichezwe Jumapili Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, imesogezwa mbele kwa siku moja lakini makocha wa timu hizo, Miguel Gamondi na Youssouph Dabo kila mmoja amejinasibu atapata ushindi.

Kwa mujibu wa ratiba mpya iliyotolewa na Bodi ya Ligi, na taarifa kutoka klabu ya Yanga, mechi hiyo itachezwa kwenye uwanja huo majira ya saa 12:30.

Taarifa kutoka ndani ya Bodi ya Ligi imesema kuwa mechi hiyo imesogezwa mbele kutokana na kuwapo kwa mechi nyingine ya African Football League itakayochezwa hapa nchini kati ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo iliyoomba kutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Esperance de Tunis kutoka nchini Tunisia.

Kocha Mkuu wa Yanga, Gamondi alisema ana uhakika haitokuwa mechi rahisi lakini amejipanga vizuri na ana uhakika wa kuendeleza ushindi mbele ya wapinzani wao hao.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, lakini tumejipanga kuendeleza ushindi mbele yao, mechi yetu ya mwisho tulipata ushindi kutokana na ubora wetu, naamini tutaendeleza ubora wetu," alisema Gamondi.

Katika mechi ya mwisho timu hizo kukutana kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Agosti mwaka Yanga ilishinda mabao 2-0 na Gamondi alisema siku hiyo ndiyo alipojua ubora na udhaifu wa Azam.

"Niliona siku ile kipindi cha kwanza walicheza vizuri sana, na sisi kipindi cha pili tulibadilika, hivyo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >